SportPesa
TZS. 576,086,780
BET LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Jela** maisha, miaka 60 na 30 kwa kubaka wanafunzi na kulawiti
UKURASA 4



**Courtois aishutumu FIFA, UEFA**
UKURASA 23


# Nipashe

Alhamisi Oktoba 14, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580733

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com
w.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




# Usiyoyajua kuhusu Mwalimu Nyerere

• **Wanazuoni** mashuhuri, waliocheza naye wachambua yaliyojificha... *Endelea ukurasa 2, 11, 12, 13 & 14*

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### KESI YA SABAYA UHUJUMU KUSIKILIZWA MFULULIZO

KESI ya uhujumu uchumi namba 27 inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa...

UKURASA WA 5

### OFISI ZA CHADEMA ZATEKETEA KWA MOTO

WATU wasiojulikana wamevunja ofisi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Jimbo la...

UKURASA WA 19

### SERIKALI YAPATA DAWA YA UHABA WA MBOLEA

WAZIRI wa Kilimo, Prof. Aldof Mkenda, amesema serikali imepanga kufufua kampuni ya mbolea ili isaidie...



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi akizungumza kwa njia ya mtandao na mshindi wa Tuzo ya Nobel ya Fasihi, Mtanzania mwenye asili ya Zanzibar, Prof. Abdurazak Salum Gurnah, ofisini kwake Ikulu Zanzibar jana, wakati akimpongeza kwa ushindi huo. **Habari Uk. 4. PICHA: IKULU**

## Machinga mwisho Oktoba 18 Dar

UKURASA 2

# Mahakama yabariki kufungua maombi mapitio tozo miamala

UKURASA 3

**MICHEZO** **SIMBA: TUTAIVAA JWANENG KIBABE** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akishiriki sala fupi ya kumwombea aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dk. John Pombe Magufuli kwenye kaburi la marehemu, wilayani Chato, mkoani Geita, juzi. Kushoto ni Mama Janeth Magufuli na (aliyepiga magoti) ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama. **PICHA: OWM**

# Usiyoyajua kuhusu Mwalimu Nyerere

**Na Romana Mallya**

MWANASHERIA wa Kenya, Prof. Patrick Lumumba, amesema waasisi wa Afrika akiwamo Baba wa Taifa la Tanzania, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, walilenga kujenga mataifa ambayo yatakuwa na umoja wa kujiendeleza kisiasa, kiuchumi na kudumisha amani.

Prof. Lumumba aliyasema hayo jana wakati wa kongamano la kumbukizi ya Mwalimu Nyerere lililofanyika mjini Chato mkoani Geita na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali.

Akizungumzia demokrasia, Prof. Lumumba alisema lazima wafahamu nchi za Afrika zilibuniwa na zile za Bara la Ulaya.

Alisema baada ya nchi za Afrika kushikwa na kutawaliwa kimabavu, wanaharakati katika nchi za kiafrika walijitolea kurejesha uhuru akiwamo Mwalimu Nyerere.

"Wakati ule wanaharakati hawa waliposhiriki katika vita dhidi ya vile vya kikoloni, nchi nyingi ambazo zilikuwa zinatawala hazikuwa na lengo la kuruhusu nchi za Afrika zijitawale, nchi mbalimbali zilikuwa na vita na watu wengi wakapoteza maisha.

"Hivi sasa tupo katika ukoloni mamboleo, tukiangazia suala la uhuru, tuna uhuru wa kisiasa, tuna wimbo wa taifa, bendera na kaulimbiu lakini katika nyanja ya uchumi bado tunaelekezwa kutoka nchi mbalimbali za Ulaya, China. Swali tunalojiuliza leo 'Je, demokrasia ni nini?"

Alisema Rais wa kwanza Ghana, Kwame Nkrumah aliwahi kueleza kuwa, mkoloni habadiliki ila anachofanya ni kubadilisha mbinu na hata akibadilika atahakikisha amewadhalilisha na kuwanyanyasa.

Pia alisema kiongozi huyo alisisitiza kuwa, Waafrika lazima watambue kwamba lengo litatimizwa tu ikiwa watajikinga na kujilinda na dhidi ya harakati hizo.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, alisema taifa ambalo halijui historia yake limefilisika, ni maskini na halina mtaji kwa sababu historia ya taifa ni kitu cha msingi.

"Tunatakiwa kuwa na wivu wa taifa letu, tusikubali taifa hili liondoke katika misingi hiyo iliyoachwa na waasisi wa taifa letu," alisema.

Aliyewahi kuhudumu kama waziri katika serikali ya awamu ya kwanza na nafasi nyingine ikiwamo kuwa Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki, Getrude Mongela, alisema wanamkumbuka Mwalimu Nyerere kwa raha na majonzi wameweka pembeni.

"Nguvu niliyonayo inatokana na malezi kutoka wa wazazi wangu, jamii niliyokulia, kutoka kwa wenzangu niliokutana nao katika maisha na kutoka kwenye kushirikiana na binadamu wenzangu ndani na nje ya taifa," alisema.

# Mume, mke wauawa jaribio wizi pikipiki

**Na Thobias Mwanakatwe,** SONGWE

MUME na mke wameuawa na wananchi wenye hasira baada ya kumvamia mwendesha bodaboda na kumpora pikipiki yake.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Janethy Mngomi, alisema tukio hilo lilitokea jana saa 10:00 alfajiri, katika kijiji cha Hatelele, Kata ya Shiwinga Mji Mdogo wa Mlowo.

Alisema watu hao (marehemu) ambao majina yao hayajafahamika walimkodi mwendesha bodaboda, Tailos Simwangwa (30) mkazi wa Mlowo na kwenda naye upande wa relini kata ya Shiyunga.

Magomi alisema baada ya kufika eneo la relini, watu hao walimkaba mwendesha bodaboda huyo na kumjeruhi kwa kumpiga na nondo kisha kumpora pikipiki yake yenye namba C 243 AXS aina ya Kinglion.

Alisema pamoja na kukabwa na kupigwa, mwendesha bodaboda huyo alipiga kelele kuomba msaada ndipo wananchi wakajitokeza na kuwavamia waporaji hao.

Kamanda Mngomi alisema wananchi walianza kuwapiga watu hao kwa marungu na mawe hadi kusababisha vifo vyao.

Alisema mwendesha bodaboda hivi sasa amelazwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Songwe na kwamba hali yake si nzuri kwa kuwa anatokwa na damu masikioni, puani na mdomoni.

Kamanda Mngomi aliwaonya wananchi kuacha kujichukulia sheria mkononi na badala yake wanapoona tukio watoe taarifa polisi ili hatua za kisheria zichukuliwe kwa wahusika.

# Machinga mwisho Oktoba 18 Dar es Salaam

**Na Waandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala, amesema mwisho wa wafanyabiashara wadogo, maarufu machinga, kuondoka kwenye maeneo yasiyo rasmi ni Oktoba 18, mwaka huu.

Amesema siku hiyo ndiyo ukomo wa muda wa mwezi mmoja waliopewa kuondoka kwenye maeneo hayo.

Amesema anashangazwa na machinga ambao wanaendelea kufanya biashara mbele ya maduka kwenye njia za watembea kwa miguu na kuendelea kufanya biashara kiholela kwa kuwa Dar es Salaam haina uhaba wa maeneo ya kufanyia biashara.

Makala aliyasema hayo jana alipokutana na viongozi wa mitaa wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mji Mwema Wilaya ya Kigamboni.

Alisema machinga ndio chanzo cha uchafu katika mkoa huo wa kibiashara kutokana na kufanya biashara kiholela na kwamba ni sehemu ya vikwazo kwa mkoa kufanya usafi, akiwataja machinga waliopo eneo la Msimbazi, Kariakoo na kuziba njia za watembea kwa miguu, kuanza kuondoka.

"Machinga wanaojijua wapo mbele ya taasisi za umma, shule, hospitali, chuo, hifadhi ya barabara, waondoke. Tulitoa muda kuanzia Septemba 17, mwaka huu, mwisho Oktoba 18 mwaka huu," alisema Makala.

Alisema maeneo mengi ya mkoa yamejaa vibanda vilivyojengwa bila mpangilio ikiwamo kwenye mitaro ya kupitishia maji ya mvua.

Alisema wafanyabiashara hao wameendelea kukiuka amri ya mkoa licha ya mabango yenye matangazo kuwekwa kwamba ni marufuku kufanya biashara kwenye maeneo hayo.

"Imeelekezwa na Rais kwamba wakuu wa mikoa na wilaya tuwapange machinga, waziri mkuu aliitisha kikao kwamba viongozi wa machinga nchini na wakuu wa mikoa wote kukutana pamoja, agizo limepokewa na limetekelezwa.

"Tulitoa mwezi mmoja kuanzia tarehe 17 mwezi uliopita, mwisho tarehe 18 mwezi huu. Ninapokea ujumbe wa watu wenye ulemavu wanataka kuandamana wakidai wanashindwa kufika mjini kwa baskeli maalum, sababu kila njia ya watembea kwa miguu zimezibwa.

"Mtu ana duka anakuja machinga anapanga bidhaa mbele ya duka na mwenye duka atauzaje? Nimefurahi machinga wameondoka leo (jana) asubuhi walioko kivukoni kuanzia Magereza hadi mwendokasi na wengine muige mfano huo kuhama kwenda maeneo rasmi, kuna baadhi wanasema hao msiwaguse hao ni wapigakura wetu, hatutafika tukisema hivyo," alionya.

Mwenyekiti wa Wenyeviti wa Serikali za Mitaa Mkoa wa Dar es Salaam, Juma Mwingamno, aliahidi kushirikiana na wenyeviti wa serikali za mitaa kuelimisha wananchi juu ya chanjo na tahadhari za kujikinga na corona.

Alisema atafanya kazi yake kwa kwa kufuata maagizo yote yaliyotolewa na mkuu wa mkoa huo ikiwamo kusimamia kila mwananchi kulipa ada ya ulinzi shirikishi.

**■Imeandikwa na Christina Mwakangale na Shufaa Lyimo**

## HABARI KITAIFA

# Mahakama Kuu yabariki mapitio tozo za miamala

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam, imekubali Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), ifungue maombi ya kuiomba ifanye mapitio ya sheria ya mfumo wa taifa wa malipo pamoja na kanuni zake zilizoweka tozo katika miamala ya fedha kwa njia ya simu.

Kadhalika, mahakama hiyo imesema imeruhusu LHRC kufungua maombi kwa kuwa wamekidhi vigezo vya kufungua maombi hayo kama walivyoomba.

Uamuzi huo ulitolewa jana na mahakama hiyo iliyoketi chini ya Jaji John Mgeta.

Alisema mahakama yake baada ya kusikiliza hoja za LHRC na Wakili wa Serikali Mkuu, Gabriel Malata, imeona kituo hicho kimetimiza vigezo vinavyotakiwa kufungua maombi hayo.

"Mahakama hii imeruhusu LHRC kufungua maombi yao kwamba wamekidhi vigezo vya kufungua maombi hayo," alisema Jaji Mgeta.

Akifafanua uamuzi wake, jaji alisema LHRC imezingatia kufungua maombi hayo ndani ya muda kama matakwa ya kisheria yanavyotaka, kabla ya miezi sita kupita tangu sheria husika ilipotangazwa. Alisema sheria ilipotangazwa na waziri Juni 30, mwaka 2021 na LHRC ilifungua shauri hilo Julai 27, 201 na hakuna ubishi hata kwa pande zote mbili kuwa maombi hayo yaliwasilishwa ndani ya muda.

Jaji alisema kigezo cha pili ni kama mleta maombi ana hoja za msingi ambazo anataka zizungumzwe katika maombi yake.

Alisema waliangalia maombi ya LHRC, kiapo na maelezo yanayounga mkono maombi hayo na alikubali kwamba LHRC wana hoja za msingi.

Kigezo cha tatu ni kama mleta maombi ana maslahi katika shauri husika na Jaji alisema kwa mujibu wa kiapo cha mleta maombi imeelezwa kwamba wamiliki simu za mtandao wa Tigo, Airtel na Vodacom ambazo anazitumia kutuma na kupokea fedha na kwamba ameathirika na sheria hiyo.

Jaji alisema kwa maana hiyo anaona mleta maombi ana hoja, anapaswa asikilizwe na LHRC imekidhi vigezo vitatu na ameruhusiwa kuleta maombi yake mahakamani.

LHRC ilifungua shauri hilo dhidi ya Waziri wa Fedha na Mipango, Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG).

Katika shauri hilo LHRC inaomba mahakama ifanye mapitio kuhusu sheria ya mfumo wa taifa wa malipo pamoja na kanuni zake zilizoweka tozo katika miamala ya fedha kwa njia ya simu.

Shauri hilo lilitokana na kupitishwa kwa mapendekezo ya bajeti ya serikali ya mwaka 2020/2021 na Sheria ya Fedha iliyosababisha kuweka tozo ambayo anaitaja kuwa mzigo kwa wananchi wa kawaida na wafanyabiashara ndogondogo.

# Kesi ya Sabaya uhujumu kusikilizwa mfululizo

**Na Allan Isack,** ARUSHA

KESI ya uhujumu uchumi namba 27 inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya na wenzake sita, imepigwa kalenda hadi Oktoba 18, mwaka huu, itakaposikilizwa mfululizo kwa wiki nzima.

Ole Sabaya na wenzake, wanakabiliwa na mashtaka matano katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, likiwamo la matumizi mabaya ya madaraka, utakatishaji wa fedha, kujihusisha na vitendo vya rushwa, kuongoza genge la uhalifu na kujihusisha na vitendo vya rushwa.

Mbali na Ole Sabaya, washtakiwa wengine katika shauri hilo ni Silvester Nyengu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31).

Akizungumza mahakamani huko jana, Hakimu wa Mahakama hiyo, Patricia Kisinga, alisema ameahirisha shauri hilo hadi Oktoba 18, mwaka huu na litasikilizwa mfululizo kwa wiki nzima.

"Kesi imeahirishwa kusikilizwa hadi Oktoba 18, mwaka huu, na kesi hii itasikilizwa kwa wiki nzima mfululizo," alisema Hakimu Patricia. Wakili wa Jamhuri, Neema Mbwambo, alidai shauri hilo lilikwenda kwa ajili ya kutajwa na aliiomba mahakama kupanga tarehe ya kusikilizwa kwa kesi.

Katika kesi hiyo, shtaka la kwanza ni la kuongoza genge la uhalifu kinyume cha sheria ya uhujumu uchumi kifungu cha 57(1) na 60(2) na linawakabili washtakiwa wote.

Ilidaiwa mahakamani huko kwamba Januari 22, mwaka huu, katika maeneo tofauti ya Jiji la Arusha, akiwa mtumishi wa serikali kwa nafasi ya Mkuu wa Wilaya ya Hai, Ole Sabaya na wenzake walifanya vitendo vya uhalifu kwa kujipatia fedha kiasi cha Sh. milioni 90 kwa manufaa yao.

Shtaka la pili ni la kujihusisha na vitendo vya rushwa na linamkabili mshtakiwa wa kwanza peke yake. Ilidaiwa mahakamani huko kwamba Januari 22 mwaka huu, eneo la kwa Murombo jijini Arusha, Ole Sabaya alijihusisha na vitendo vya rushwa kwa kumtaka Francis Mroso kumpatia fedha kiasi cha Sh. milioni 90 kwa kumshinikiza ili asitoe taarifa za jinai za mtu huyo za madai ya ukwepaji kodi.Shtaka la tatu ni la kujihusisha na vitendo vya rushwa na linamkabili mshtakiwa wa kwanza peke yake. Inadaiwa kwamba Januari 22, mwaka huu, Ole Sabaya akiwa katika eneo la kwa Morombo jijini Arusha, alijihusisha na vitendo vya rushwa kwa kujipatia fedha kiasi cha Sh. milioni 90 kutoka kwa Francis Mroso, ili asitoe taarifa za jinai za mtu huyo za madai ya ukwepaji kodi.

Shtaka la nne ni la matumizi mabaya ya madaraka na linamkabili Ole Sabaya peke yake. Inadaiwa kuwa Januari 22 mwaka huu, Ole Sabaya, akiwa katika eneo la kwa Murombo jijini Arusha, alitumia vibaya nafasi yake ya Mkuu wa Wilaya ya Hai, alimtisha Francis Mroso kumfungulia mashtaka ya kukwepa kodi.

SHIRIKA LA BIMA LA TAIFA (NIC)

SISI NDIYO BIMA

KUMBUKIZI YA MIAKA 22 YA KIFO CHA BABA WA TAIFA MWALIMU JULIUS KAMBARAGE NYERERE

Bodi ya Wakurugenzi, Uongozi na Wafanyakazi wote wa Shirika la Bima la Taifa (NIC). Tunaungana na Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan, Familia ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Watanzania wote katika kumbukizi ya Miaka 22 ya Kifo cha Baba wa Taifa.

Karibu Tukuhudumie
#SisiNdiyoBima



S.L.P 9264, Dar es Salaam, Tanzania
Baruapepe : info.nic@nictanzania.co.tz
Simu : +255 222113824/6

Baruapepe :info.nic@nictanzania.co.tz
Tovuti :www.nictanzania.co.tz
Namba ya Bure :0800110041

nic_tanzania

21651082

HABARI KITAIFA

# Jela maisha, miaka 60 na 30 kubaka wanafunzi na kulawiti

**Na Waandishi Wetu**

WATU watano, wakiwamo babu na mjukuu, wamehukumiwa vifungo vya maisha, miaka 60 na 30 jela baada ya kukutwa na makosa ya kubaka na kuwapa ujauzito wanafunzi pamoja na kulawiti.

Katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mbeya, dereva wa Bajaj, Deus Peter (25) Mkazi wa VETA jijini humo, amehukumiwa kifungo cha miaka 30 jela baada ya kupatikana na hatia ya kumbaka  na kumsababishia ujauzito mwanafunzi wa kidato cha nne, hivyo kukatisha masomo yake.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi na Hakimu Mkazi Andrew Scout, baada ya mshtakiwa kufikishwa mahakamani na kusomewa mashtaka mawili na kukiri kutenda makosa hayo.

Akisoma mashtaka hayo katika  kesi  namba 59 ya mwaka 2021, Wakili wa Serikali, Hebel Kihaka akisaidiana na Zena James alidai kuwa kwa nyakati tofauti  kati ya Septemba 2020 na Aprili 2021, mshtakiwa alimbaka mwanafunzi wa shule moja ya sekondari (jina la mwanafunzi na shule vinahifadhiwa) kinyume cha kifungu namba 130(1)(2)(e) na 131(1) cha Kanuni ya Adhabu sura ya 16 kilichofanyiwa marekebisho mwaka 2002.

Kosa la pili ni kijana huyo ni kumsababishia ujauzito mwanafunzi huyo kinyume cha kifungu cha 60 A (3) cha cha Sheria ya Elimu Sura ya 353.

Baada ya kusomewa mashtaka hayo mawili, upande wa mashtaka uliiomba mahakama kutoa adhabu kama sheria inavyoelekeza ili iwe fundisho kwa mshtakiwa na watu wengine kwenye jamii.

Hata hivyo, mshtakiwa aliiomba mahakama mu kumpunguzia adhabu kwa kuwa bado ni kijana anayetegemewa na kosa hilo ni la kwanza na kwamba anajutia makosa hayo.

Baada ya maelezo ya pande zote, Hakimu Scout alimhukumu Peter kwenda kutumikia kifungo cha miaka 30 jela kwa kosa la kwanza na kosa la pili la kumsababishia ujauzito mwanafunzi huyo nalo atumikie kifungo cha miaka 30 jela. Hakimu alisema makosa hayo yanakwenda pamoja hivyo, atatumikia kifungo cha miaka 30.

Jijini Dar es Salaam, dereva Paul Vedastus, maarufu kama Majani (33), amehukumiwa kwenda jela miaka 60, baada ya kukutwa na hatia kumbaka na kumpa ujeuzito mwanafunzi.

Hukumu hiyo ilisomwa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Hakimu alisema mahakama yake baada ya kusikiliza mashahidi wa pande zote mbili, bila kuacha shaka imemwona mshtakiwa ana hatia katika makosa yote mawili.

Alisema kosa la kumbaka mwanafunzi, mshtakiwa atakwenda jela kutumikia kifungo cha miaka 30 na kosa la pili la kumpa mimba, pia atatumikia kifungo cha miaka 30 na adhabu zote zitakwenda sambamba.

Awali, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Mwanaamina Kombakono, alidai kuwa upande wa Jamhuri hauna kumbukumbu ya makosa ya nyuma ya mshtakiwa, aliomba mahakama kutoa adhabu kwa mujibu wa sheria.

Akitoa utetezi wake ili apunguziwe adhabu, mshtakiwa aliiomba mahakama kumpunguzia adhabu kwa kuwa ana familia inamtegema.

"Mimi ni mzazi wa watoto watatu wote wanasoma na nina wazazi wananitegemea, wagonjwa, mama yangu anasumbuliwa na kansa ananitegemea mimi na pia baba yangu ni mwanajeshi mstaafu ambaye ameathirika na ugonjwa wa Ukimwi, wote wananitegemea mimi," mshtakiwa alisema akiomba huruma ya mahakama.

Hakimu Simba alisema adhabu ya makosa kama hayo imepangwa kwa mujibu wa sheria, kwasababu ya wanafunzi wanaopewa mimba na hakuna namna ya kuibadilisha ni miaka 30 jela kila kosa.

Katika kesi ya msingi, ilidaiwa kuwa, kati ya Mei na Agosti, 2016, eneo la Tandika wilayani Temeke, jijini Dar es Salaam mshtakiwa alimbaka na kumpa mimba mwanafunzi.

Mkoani Singida, Mahakama ya Wilaya ya Singida, imemhukumu kifungo cha maisha jela, mkazi wa Mtaa wa Mizani,Kata ya Mandewa, mkoani Singida, Hamisi Shabani (25), kwa makosa ya kubaka na kulawiti.

Aidha, Mahakama hiyo pia imemhukumu adhabu ya kifungo cha nje cha mwaka mmoja, Shabani Rajabu (17), mkazi waa Mtaa wa Mizani, Manispaa ya Singida baada ya kumtia hatiani kwa makosa ya kubaka na kulawiti.

Rajabu amehukumiwa kifungo cha nje kutokana na kusimamiwa na sheria ya watoto kutokana na umri wake kutofikia miaka 18.

Hukumu ya kesi ya jinai namba 168/2020 ilitolewa na Hakimu Mkazi Mwandamizi Robert Oguda, baada ya kusikiliza mashahidi saba ambao alisema ushahidi wao haukuacha shaka.

Ilidaiwa kuwa tukio hilo lilitokea Agosti 27, mwaka jana, majira ya saa za usiku, mtaa wa Mizani, Kata ya Mandewa, Manispaa ya Singida ambapo washitakiwa huyo alikuwa akiishi nyumba moja na mwanamke huyo waliyembaka na kumlawiti.

Ilidaiwa mahakamani humo kuwa siku ya tukio walinunua pombe ya kienyeji na kumkaribisha mwanamke na kuanza kunywa pamoja hadi alipolewa, na kumfanyia kitendo hicho kwa zamu.

**BABU NA MJUKUU**

Mahakama ya Wilaya ya Chato, mkoani Geita, imewahukumu watu wawili kutumikia kifungo cha maisha jela kwa kosa la kumbaka mwanafunzi wa darasa la sita mwenye miaka 16 na kumsababishia maumivu makali.

Waliohukumiwa vifungo hivyo ni Fabiani Filipo (22) na Thomas James (48) wote ni wakazi wa Kijiji cha Kasala Wilaya ya Chato.

Hukumu hiyo imetolewa jana na Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Erick Kagimbo, baada ya ushahidi kuthibitisha kosa hilo pasipokuacha shaka yoyote na kuwatia hatiani washtakiwa hao.

Katika kesi hiyo, upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Clemence Mango alipeleka mashahidi wanne na kielelezo kimoja ambavyo vilithibitisha kuwa washtakiwa hao walimbaka mwanafunzi huyo ambaye jina lake limehifadhiwa.

Akisoma huku hiyo, Hakimu Kagimbo alisema mshtakiwa wa pili Thomas James alimchukua mwanafunzi huyo na kumpeleka katika Kijiji cha Kasala, wilayani Chato kwa mjukuu wake ambaye ni mshtakiwa wa kwanza Fabiani Filipo kwa lengo la kumuozesha.

Aidha alisema baada ya kufika katika Kijiji cha Kasala mshtakiwa wa pili ambaye ni babu wa mshtakiwa wa kwanza alimkabidhi mjukuu wake mwanafunzi huyo na kuishi naye kama mke wake kuanzia mwenzi wa tatu hadi mwezi wa nane mwaka 2020.

**Imeandikwa na Grace Mwakalinga (MBEYA), Hellen Mwango (DAR), Jumbe Ismailly (SINGIDA) na Joctan Ngelly (CHATO).**






# Dk. Mwinyi amwita Z'bar mshindi tuzo ya Nobel

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amempongeza mshindi wa tuzo ya Nobel katika fasihi, Profesa Abdulrazak Gurnah (Pichani), na kumkaribisha rasmi Zanzibar.

Dk. Mwinyi alitoa mwaliko kwa mshindi huyo wakati akizungumza naye mbashara kwa njia ya mtandao.

"Kwanza, ninataka nichukue fursa hii nikupe hongera, nikupe pongezi nyingi kwa kupata 'Nobel price' na sisi tumechukulia kama ni fahari kwetu sote Wazanzibar, Watanzania na Waafrika kwa jumla.

"Nichukue fursa hii nikukaribishe uje Zanzibar, sehemu ulipozaliwa na ambapo ndipo nyumbani. Kwa hiyo, kwa sababu na sisi tunajifaharisha kwa mafanikio yako, basi tunaona ni vizuri tukakupa mwaliko rasmi ukipata wasaa wakati wote, basi karibu nyumbani.

"Leo kwa kweli nilikuwa na hayo mawili, la kwanza kukupongeza na la pili kukukaribisha rasmi," Dk. Mwinyi alisema.

Katika mazungumzo yao hayo, Prof. Gurnah alisema ushindi huo ni wa Watanzania wote na waandishi wote wa vitabu.

Profesa Gurnah alishukuru kwa mwaliko huo kutoka kwa Dk. Mwinyi na yuko tayari kwenda Zanzibar wakati wowote.

Mwandishi huyo wa riwaya, alishinda tuzo ya amani ya Nobel ya mwaka 2021 katika fasihi inayotolewa na Sweedish Academy ambao ndio waandaaji.

Miongoni mwa zawadi alizojinyakulia Prof. Gurnah baada ya kushinda tuzo hiyo ni medali ya dhahabu pamoja kitita cha Dola za Marekani milioni 1.14 ambazo ni zaidi ya Sh. bilioni 2.6.



# MOI yafanya upasuaji wa migongo iliyopinda

Na Mary Geofrey

TAASISI ya Tiba ya Mifupa (MOI) inatarajiwa kuhudumia watoto 10 wenye tatizo la kupinda mgongo (scoliosis) katika kambi maalum ya mafunzo na upasuaji iliyoanza kufanyika jana.

Kambi na mafunzo hayo imeratibiwa na MOI kwa kushirikiana na Hospitali ya Chuo Kikuu cha Well Cornell cha Marekani.

Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respecious Boniface, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kambi hiyo, alisema imelenga kuwajengea uwezo madaktari wa Tanzania na nchi zingine barani Afrika, ili kuwahudumia wagonjwa kwa ufanisi mkubwa.

"Hii ni kambi yetu ya pili, tulifanya kambi ya kwanza mwaka 2019 na mwaka 2020 hatukufanya kwa sababu ya changamoto ya UVIKO-19. Sasa ndio tumeanza tena na lengo letu ni wataalamu hawa wakiondoka tuendelee kutoa huduma hizi hapa nchini bila ya mgonjwa kulazimika kwenda nje ya nchi kufuata huduma hii," alisema Dk. Boniface

Alisema watoto 10 watapata huduma ambapo watano watahudumiwa kwa njia ya kisasa ya P.O.P na watano wengine watahudumiwa kwa upasuaji mkubwa wa kunyoosha mgongo.

Mkufunzi wa Mafunzo hayo, Prof. Alaa Ahmad kutoka Palestine, alisema ni heshima kubwa kupata nafasi ya kuja Tanzania kutoa mafunzo kwa madaktari ili waweze kuwahudumia wagonjwa kwa wakati.

Prof. Alaa alisema ana imani kubwa kwamba mafunzo haya yatawasaidia madaktari wa Tanzania, Kenya na Malawi na mataifa mengine na huduma zitaendelea kutolewa barani Afrika.

## Ofisi za CHADEMA zateketea kwa moto

Na Thobias Mwanakatwe, TUNDUMA

WATU wasiojulikana wamevunja ofisi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Jimbo la Tunduma na kuteketeza kwa moto nyaraka mbalimbali zilizokuwa ndani ya ofisi hiyo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Janeth Magomi, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa walipata taarifa za tukio hilo baada ya kupigiwa simu jana alfajiri na Katibu wa Baraza la Vijana wa CHADEMA (BAVICHA) Wilaya ya Momba, Mussa Mwaipata.

Alisema baada ya kupewa taarifa hizo, Jeshi la Polisi na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji walifika eneo la tukio walibaini ofisi hiyo kuvunjwa na kuchomwa moto kwa nyaraka mbalimbali muhimu za ofisi hiyo.

Kamanda Magomi alitaja baadhi ya vitu vilivyochomwa moto, mbali na nyaraka kuwa ni furushi la nguo ambazo zilikuwa pembezoni mwa mlango uliovunjwa.

Kutokana na tukio hilo, Magomi amewaomba wananchi wenye taarifa zozote muhimu kuhusu uharibifu huo wazitoe kwa jeshi hilo ili wote waliohusika na tukio hilo la uvunjifu wa amani wakamatwe.

"Wakati tukiendelea na uchunguzi wa kiintelijensia ili kuwafahamu au kuwabaini wote waliohusika, tunaomba mwananchi yeyote mwenye taarifa aje atupatie ili wahusika wote wapatikane kwa kuwa tukio hili halikubaliki hata kidogo," alisema.

Hata hivyo, Kamanda Magomi alisema hadi kufikia jana jioni hakuna mtu yeyote aliyekamatwa au kushikiliwa na jeshi hilo kuhusiana na tukio hilo na kwamba uchunguzi wa kina unaendelea.

Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Nyasa, Joseph Mwasote, maarufu China, alisema watatoa taarifa rasmi leo kuhusu tukio hilo.

## ATCL kuanzisha safari mpya mwezi Novemba

Na Maulid Mmbaga

SHIRIKA la Ndege Tanzania (ATCL) limezindua safari za anga za kwenda mikoa ya ndani pamoja na nje ya nchi baada ya kusitishwa kwa muda na zinatarajiwa kuanza rasmi mwezi Novemba, mwaka huu.

Uzinduzi huo unatokana na ujio wa ndege mpya mbili, Airbus A220-300 za shirika hilo zilizopokelewa Zanzibar wiki iliyopita, ambazo zimetajwa kusaidia katika kuongeza wigo wa safari za anga nchini.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano (ATCL), Josephat Kagirwa, alisema kwa safari za ndani zitafanyika kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza kupitia Dodoma kuanzia Novemba 5 na Dar es Salaam kwenda Mtwara, Novemba 10, mwaka huu.

Alisema safari za nchi jirani ikiwamo kutoka Dar es Salaam kwenda Bunjumbura-Burundi, zitaanza Novemba 8, Lubumbashi-Congo na Ndola-Zambaia, Novemba 18, Nairobi-Kenya, Novemba 26, na safari za mizigo kwenda China zitakuwa zikifanyika mara moja kwa wiki kila Ijumaa.

"Mafanikio hayo ya kuongeza safari yametokana na ushirikiano wetu na serikali katika uwekezaji na utekelezaji wa mpango mkakati wa miaka mitano iliyowekwa na shirika kuanzia 2017 hadi 2022 kwa dhumuni la kuiendeleza kampuni.

"Pia tunaishukuru serikali kwa kuendelea kutuunga mkono na kuendelea kuongeza nguvu katika usafiri wa anga na ndege zilizofika zina uwezo wa kubeba abiria 132, lakini pia zimeboreshwa kwa kuwezeshwa kubeba tani 69.9 ikilinganishwa na zingine zilizokuwa zinauwezo wa tani 67.6," alisema Kagirwa.

Vile vile, alisema ndege hizo pia zimeongezewa uwezo wa kumsaidia rubani kufanya kazi zake kirahisi na zinaweza kufanya safari kwa saa sita bila kutua na kwamba ujio wake umewawezesha kufikiria kupanua wigo zaidi wa safari za nje.


TRA

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

MIAKA 22 YA KUMBUKUMBU YA KIFO CHA BABA WA TAIFA MWALIMU JULIUS KAMBARAGE NYERERE



216512502

## MAONI & UCHAMBUZI

**Nipashe**
MWANGA WA JAMII

# Maono ya Nyerere yafuatwe kwa vitendo

**BABA** wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, wakati wa uhai wake hususan akiwa Rais wa Taanganyika na baadaye Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alianzisha na kutekeleza mipango mingi, ambayo iliiwezesha nchi yetu kusimama kama taifa.

Baada ya nchi kupata Uhuru wa bendera mwaka 1961, alibaini kuwa bado kulikuwapo na kazi zaidi ya kufanya kutokana na mfumo wa uchumi tuliourithi kutoka kwa wakoloni kutoonyesha dalili kama ungewapa matunda wananchi.

Hiyo ni kutokana na njia zote kuu za uchumi kama ardhi, viwanda, migodi, shule, hospitali na za usafirishaji kuendelea kuwa chini ya umiliki wa watu wachache. Kadhalika, ajira zilikuwa ni shida kwa wazalendo.

Aliamua kutaifisha mali hizo zote na kuziweka chini ya umiliki wa serikali, lengo likiwa ni kuwawezesha Watanzania wote kunufaika na kupata maendeleo. Mbali na utaifishaji, Mwalimu Nyerere pia aliunda mashirika ya umma takribani 500 ambayo pamoja na kufanya shughuli za uzalishaji na kuingiza fedha za ndani na za kigeni, yalisaidia sana kuwapa ajira wananchi wengi wakiwamo hata ambao hawakuwa na elimu kubwa.

Hatua nyingine alizochukua ni kutoa bure huduma za kijamii kwa wananchi kama elimu, matibabu, maji na nyinginezo. Katika kuhakikisha kwamba huduma hizo zinawafikia wananchi wengi, alianzisha 'operesheni vijiji' mapema miaka ya sabini, ambapo wananchi walikusanywa na kupelekwa kwenye vijiji maalum vilivyowekewa huduma hizo. Mwalimu Nyerere aliona njia ambayo ingeifikisha Tanzania katika maendeleo ni kufuata itikadi ya Ujamaa na Kujitegemea akiamini kuwa ni itikadi ambayo haina matabaka na inayoweza kuwafanya watu wote kunufaika na keki ya taifa, lakini kumfanya kila mmoja aishi kwa kufanya kazi kupitia kilimo. Kwa kuamini kuwa asilimia kubwa ya wananchi waliishi kwa kutegemea kilimo, serikali iliweka msukumo mkubwa kwa sekta hiyo ikiwamo kugawa pembejeo bure, kupeleka maofisa ugani vijijini na kuyatafutia masoko mazao yote ya biashara.

Maazimio kadhaa yalitangazwa ikiwa ni njia ya kutekeleza kwa vitendo sera ya Ujamaa na Kujitegemea yakiwamo la Arusha la mwaka 1967 ambalo lililitumika kuweka njia zote za uchumi kwa umma; la Musoma Elimu kwa Wote 1974 na la Iringa Siasa ni Kilimo mwaka 1972. Leo tunapofanya kumbukizi ya miaka 22 ya kifo cha Mwalimu Nyerere tunaona mchango wake mkubwa na alivyojitoa katika historia na maendeleo ya nchi yetu.

Kuna mengi ya kumkumbuka Nyerere, lakini safu hii haiwezi kuyabeba yote ila baadhi ya mengine ni utaratibu wake na viongozi wenzake kwenda vijijini kila mara kuhimiza kilimo pamoja na kuwaunganisha Watanzania kuwa wamoja bila kuegemea kwenye ukabila, ukanda na udini. Maisha ya Mwalimu Nyerere yanapaswa kuwa kioo kwetu, hivyo hatunabudi kuendeleza yote mazuri aliyotuachia.


Tunaelewa kuwa mfumo wa uchumi umebadilika kutokana na kutawaliwa na utandawazi, lakini hilo halitafuta kabisa maono aliyokuwa nayo Nyerere. Kama wakati wake alijielekeza kwenye kilimo, kwa nini sasa viongozi wetu wakaweka nguvu kubwa katika ujenzi wa viwanda kukabiliana na tatizo la sasa la ajira kwa vijana wanaohitimu vyuo vikuu?

Tunaona pia kuwapo kwa umakini mkubwa katika kubinafsisha baadhi ya mashirika ya umma kuepuka makosa yaliyofanyika miaka iliyopita, hivyo kuisababishia nchi hasara.

Wakati nchi yetu inapata Uhuru, Mwalimu Nyerere aliwataja maadui watatu kwa taifa letu ni umaskini, ujinga na maradhi. Hata hivyo wanazuoni kwa sasa wameongeza adui mwingine kuwa ni ufisadi. Tunawashauri viongozi wetu kwamba mawazo mengi ya Nyerere hayajafa, hivyo katika kuwaletea maendeleo wananchi, hawanabudi kuendelea kuyafuata. Msisitizo uwe wa kupambana na maadui hao ukwamo wizi na matumizi mabaya ya fedha za umma.

Licha ya serikali kuacha kutoa huduma bure za kijamii kutokana na masharti ya wakubwa wa dunia mwanzoni mwa miaka ya tisini, ni jambo la kujivunia kuona serikali imefuta gharama za elimu ya msingi hadi kidato cha nne.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Nikigeukia penye afya, pia elimu, namuona Nyerere

**KARIBU** maeneo yote nchini kuna ujenzi wa zahanati kila kijiji, ujenzi wa vituo vya afya kila kata na hospitali kila wilaya, huku mikoa ina Hospitali za Rufani, penye kanda kuna rufani kuu na ngazi kuu kabisa ni Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Huo ni muundo wa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Taifa (MMAM) ya mwaka 2007, lakini ukaanza mwaka uliofuata kutokana na kuelemewa muda wa maandalizi, sasa unaobeba tafsiri ya kuhakikisha Watanzania wanapata huduma za afya jirani waliko.

Uboreshaji huo wa huduma za afya, unalenga kupambana na maradhi, ambayo ni miongoni mwa maadui watatu waliotangaziwa vita na Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere, baada ya nchi kupata uhuru.

Maadui wengine walikuwa ni ujinga na umaskini, ambao kila mmoja aliandaliwa mikakati ya kumdhibiti, ili Watanzania wawe huru kutoka kwa maadui hao.

Kwa kuwa maendeleo yanaletwa na wenye afya njema, Mwalimu Nyerere alihakikisha afya inapewa kipaumbele kwa kuboresha miundombinu yake, kuanzia ujenzi wa zahanati, vituo vya afya na hospitali zikiwamo za rufani.

Pia iligusa kata kuwa zote kupatiwa vituo vya afya, wilaya kuwa na hospitali, ambayo ni mkakati wa kusogeza huduma za afya karibu na wananchi waliko, ili kuwaondolea adha ya kusafiri umbali mrefu, kufuata huduma hizo.

Nikirejea katika hatua zinazochukuliwa na serikali sasa za uboreshaji huduma za afya kwa kuzisogeza karibu na wananchi, ni wazi zinaenzi vitendo na ndoto za Mwalimu Nyerere, kuondoa adui maradhi.

Niseme kwamba, ni muktadha ambao Mwalimu Nyerere aliupa mkazo kuondoa adui maradhi na inaendelea kufanywa kwa vitendo, hasa kwa kusogeza huduma za afya karibu na wananchi wa maeneo mbalimbali nchini.

Wakati leo tuna kumbukumbu ya 22 kifo cha Rais huyo wa kwanza, ni vyema kila mmoja akatimiza wajibu wake kwenye eneo lake la kazi, ili kuharakisha mikakati ya serikali ya kuboresha huduma za afya.

Ni muhimu ikumbukwe, ili mtu awe na nguvu za kufanya kazi na kujiletea maendeleo, kuna ahaja ya afya njema, hivyo suala la kuwa na zanahati, vituo vya afya na hospitali zikiwamo za rufani, zina umuhimu mkubwa.

Pia ni dalili tosha za vita dhidi ya adui maradhi, kuwapo shule nyingi za msingi, sekondari na vyuo, ikiwa ni dalili nyingine ya kupambana na adui ujinga.

Aidha, panapokuwapo shughuli za kiuchumi, inaweka dalili za kuondokana na adui umaskini. Vyote kwa ujumla wake, binafsi ninaona kiashiria ya kile Mwalimu alichokusudia kwa Watanzania, kinaendelea kutimia.

Uongozi wake Nyerere, alisimamia kaulimbiu ya 'Uhuru ni Kazi.' Rais wa sasa Samia Suluhu Hassan, amekuja na 'Kazi Iendelee', kwamba Watanzania waendelee kuchapa kazi kama watu huru katika nchi yao.

Hayo ndiyo yalikuwa maono yake Mwalimu kwa Tanzania, kwamba wawe na afya njema, uelewa, pia kufanya kazi ili kuondokana na umaskini. Ndivyo serikali zilizofuata baada yake zinaendelea kufanya.

Katika hilo la kupambana na adui ujinga, historia inaonyesha namna alivyohakikisha kila mtoto wa Kitanzania, anapata elimu tena bure, mfumo ambao sasa serikali imerejesha tena nchini kama ilivyokuwa enzi ya uongozi wake ili watu wengi wapate elimu.

Alihakikisha watoto nchini wanapata elimu sahihi, kwa kuwa ndiyo mkombozi wa kuwatoa katika dimbwi la umaskini, pia kupambana na maradhi mbalimbali.

TANGAZO


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi
**WAKALA YA BARABARA TANZANIA**




**KUMBUKUMBU**

Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi, Mtendaji Mkuu, Menejimenti na Wafanyakazi wa Wakala ya Barabara Tanzania (**TANROADS**), tunaungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Samia Suluhu Hassan** na Watanzania wote katika kumbukumbu ya **miaka 22** ya kifo cha Baba wa Taifa na Rais wa awamu ya kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mwalimu Julius Kambarage Nyerere** kilichotokea **Oktoba 14, 1999** katika hospitali ya Mtakatifu Thomas nchini Uingereza. ***TANROADS,*** tutaendelea kukuenzi kwa vitendo kwa kujenga miundombinu bora kwa maendeleo ya Taifa.



**TANROADS Makao Makuu**
**Ghorofa ya 1-3, 10 Barabara ya Shaaban Robert / Garden Avenue**
**S.L.P 11364 Dar Es Salaam**
**Baruapepe:Tanroadshq@tanroads.go.tz**

**www.tanroads.go.tz**

**MIUNDOMBINU BORA YA BARABARA, MADARAJA NA VIWANJA VYA NDEGE KWA MAENDELEO YA TAIFA**

216512902

## Mbunge awataka wananchi kushiriki miradi maendeleo

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MBUNGE wa Jimbo la Kibaha Mjini, Silvestry Koka, amesema ataendelea kuchangia miradi ya maendeleo kwenye maeneo ambayo wananchi wameanza kuonyesha jitihada zao ili kuwapa motisha wa kufanyakazi kwa bidii.

Akizungumza hivi karibuni na wananchi wa Kata ya Visiga baada ya kukagua miradi mbalimbali, alisema ni muhimu ukawapo ushiriki wa wananchi kwenye miradi ya maendeleo ambayo moja kwa moja itawanufaisha.

Aliahidi kuchangia shilingi milioni tano kwa miradi hiyo ili ikamilike na kuondoa vikwazo vya maendeleo kwa wananchi.

Kwa mujibu wa Koka, wananchi wenye nia ya kubadilika kimaendeleo wanatakiwa kuonyesha jitihada katika kuchangia nguvu kazi pamoja na fedha za kuanzia, ili kurahisisha wenye lengo la kusaidia kuchangia fedha na vifaa.

"Nimechangia shilingi milioni mbili ujenzi wa vyumba vya madarasa shule ya msingi Saeni nimekuta wameanza msingi tayari wananchi wamechangia Sh. milioni 3.5 naunga mkono kuwapunguzia wanafunzi wa maeneo yale kutembea umbali mrefu," alibainisha.

Mbunge huyo alichangia shilingi milioni mbili ujenzi wa jengo la kujifungulia katika Zahanati ya Visiga na Shilingi milioni moja ujenzi wa karavati mtaa wa Gaza na Jerusalemu.

Koka aliahidi kuweka utaratibu wa kufanya mikutano na wananchi mara kwa mara kutatua kero za maji, elimu na afya kwenye kila kata.

Naye Diwani wa Visiga, Mbegu Kambi alimshukuru mbunge huyo kwa namna alivyojitoa kusaidia fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Mbegu alisema ujenzi wa Shule ya Msingi Saeni utawaondolea adha wanafunzi kutembea umbali wa kilomita 10 kwenda katika Shule ya Msingi Visiga. Alibainisha kuwa tayari halmashauri imetenga kiasi cha Sh. milioni 20 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule hiyo, kwenye mtaa ambao unakadiriwa kuwa na wakazi zaidi ya 300.

Pia, alisema wakazi wa Gaza na Jerusalemu walikuwa wakikumbana na adha ya kushindwa kuvuka kwenda mtaa wa pili kipindi cha mvua na wananchi tayari wamechangia Sh. 800,000 kati ya 2,500,000 zinazohitajika kujenga kalavati hilo.



Meneja Mwandamizi, Idara ya Wateja Binafsi wa Benki ya NMB, Ally Ngingite (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, wakati wa kuchezesha muhula wa pili wa bahati nasibu ya Bonge la Mpango, jijini Dar es Salaam jana, ambapo wateja wawili walijinyakulia pikipiki za miguu mitatu za mizigo kila mmoja na 10 walijinyakulia 100,000/- kila mmoja. Kushoto ni Ofisa wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT), Joram Mtafya na Ofisa Huduma kwa Wateja wa benki hiyo, Neema Kazoviyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bil. 90/- za Samia kuboresha miundombinu hifadhi za taifa

**Na Lusungu Helela**

WIZARA ya Maliasili na Utalii imesema Sh. bilioni 90.2 ilizopewa kutoka kwenye fungu la mapambano dhidi ya corona kati ya Sh. trilioni 1.3 kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF) zitatumika kununulia vifaa vya kupima ugonjwa huo na kuboresha miundombinu katika maeneo ya hifadhi.

Pia imesema fedha hizo zitatumika kwa ajili ya mafunzo kwa wadau wa utalii wakiwamo madereva wa magari ya watalii, waongoza watalii, wabeba mizigo na wahudumu wa hoteli za kitalii.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, jana jijini hapa wakati wa mkutano wa Wizara ya Maliasili na Utalii na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF). Mkutano huo ulilenga kuzitafutia ufumbuzi changamoto zinazokabili sekta ya utalii hususan katika kipindi cha corona,

Wadau mbalimbali wa utalii kutoka sekta binafsi wakiongozwa na Mwenyekiti wa TPSF, Angelina Ngalula, walishiriki mkutano huo wakiwamo wanachama wa Chama cha Waongoza Watalii Tanzania (TATO), Baraza la Biashara la Taifa (TNBC), Chama cha wadau wa Utalii wa Utamaduni (TACTO) va Chama cha Wamiliki wa Hoteli Tanzania (HAT).

Dk. Ndumbaro alisema Rais Samia Suluhu Hassan ametoa fedha hizo ili kuinyanyua sekta ya utalii kutokana na janga la corona ambalo limeiacha sekta hiyo katika hali tete na kusababisha watalii wakisitisha safari kuja nchini kutembelea vivutio mbalimbali.

Alisema vifaa vitakavyonunuliwa kwa ajili ya kupimia corona, vitasambazwa maeneo yote ya vivutio vya utalii ili kuwasaidia watalii pindi watakapopimwa wapewe majibu huko huko tofauti na ilivyo sasa.

"Tumedhamiria kuondoa usumbufu ili watalii watakapokuja nchini wasipate usumbufu kwa kuhakikisha kila hifadhi inatoa huduma hizo kwa haraka ili kuwafanya watalii wasikae kusubiri matokeo kwa muda mrefu," alisema.

Kuhusu miundombinu, Dk. Ndumbaro alisema ujio wa fedha hizo utasaidia kufungua hifadhi kama vile Hifadhi ya Taifa ya Nyerere ambayo imekuwa na barabara nyingi lakini zimekuwa hazipitiki, hivyo fedha hizo zitaboresha barabara ili zipitike kipindi chote cha mwaka.

Alisema barabara zitaboreshwa huku barabara zingine zikifunguliwa katika maeneo ya hifadhi ambazo hazina miundombinu ili maeneo hayo yafikike kwa urahisi.

"Barabara ikiwa nzuri na wewe hoteli yako iko ndani sana, watalii watakuja kulala katika hoteli yako kwa sababu kuna barabara nzuri, hivyo hela hii inakwenda kufanya kazi hiyo," alisisitiza.

Mwenyekiti wa TPSF, Angelina Ngalula, alimshukuru Rais Samia kwa kujitoa kuisaidia sekta ya utalii nchini.

"Tunaomba salamu zifike kwa Mheshimiwa Rais kwa juhudi za kuendeleza utalii kwa kututafutia fedha kutoka IMF. Tumemuona anavyoipambania sekta ya utalii kupitia kipindi chake maarufu alichokiasisi cha Royal Tour ambacho kimeongeza ujasiri kwa wawekezaji wa sekta ya utalii nchini. Tunampongeza sana Rais wetu," alisema.

# MSD yafanyia kazi maagizo ya Majaliwa

**Na Mary Geofrey**

BOHARI ya Dawa (MSD) imeanza kusambaza dawa katika maeneo yote yenye uhaba wa dawa nchini, ikitarajia kukamilisha usambazi huo keshokutwa.

Usambazaji huo umeanza kufanyika muda mfupi tangu Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kumwagiza Mkurugenzi Mkuu wa MSD, Meja Jenerali Gabriel Mhidze, ahakikishe mpaka Oktoba 16 mwaka huu, dawa ziwe zimepatikana katika maeneo yote nchini.

Waziri Mkuu alisema kuwa ni maelekezo ya serikali vituo vyote vya kutolea huduma zikiwamo zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya, hospitali za rufani za mikoa lazima zipate dawa kwa kuwa zinategemea MSD.

Mkurugenzi Mkuu wa MSD, Meja Jenerali Mhidze, akizungumza na waandishi wa habari juzi jijini Dar es Salaam kuhusu utekelezaji huo, alisema walianza kusambaza mzigo tangu siku hiyo yalipotolewa maagizo hayo kwa magari mawili yenye shehena ya tani 10 kuondoka na kupeleka dawa katika maeneo ambako kulikuwa na upungufu.

Alisema dawa zinazoendelea kusambazwa zilikuwa katika bohari hiyo kuu kusubiri kusambazwa katika maeneo husika.

Alisema MSD inaendelea kusambaza dawa nchi nzima na kwamba tayari wameshapeleka Uvinza mkoani Kigoma ambako magari manne yamepeleka shehena. Alifafanua kuwa kuna gari aina ya Scania lenye tani 10 na magari madogo kwa ajili ya kupeleka maeneo ambayo magari makubwa hayawezi kuingia ikiwamo Kasulu mkoani Kigoma.

Meja Jenerali Mhidze alisema mzigo wanaousambaza ni dawa ambazo zipo kwenye bohari yao na kwamba kuna mzigo wa kontena nne kutoka Kenya na Uganda na kontena sita za shehena ya bidhaa mbalimbali ziliozingia nchini kupitia Bandari ya Dar es Salaam.

Alisema wanatarajia kupokea dawa tani 42 kutoka nchi mbalimbali na kwamba tani 24 zinatarajiwa kuawasili leo na keshokutwa na tani nyingine 18 zitawasili wakati mwingine.

Alifafanua kuingia kwa mzigo huo wa dawa nchini kutasaidia kupunguza upungufu wa dawa katika maeneo ambako kuna upungufu. Kiongozi huyo wa MSD wanazosambaza wanapitisha kwenye hospitali, zahanati na vituo vya afya nchini na hata kama wateja wao hawana fedha, huwakopesha na baadaye kurejesha.

## Watoto wenye vichwa vikubwa/ mgongo wazi wasaidiwa

**Na Mwandishi Wetu**

WATOTO wenye changamoto ya kiafya ya vichwa vikubwa na mgongo wazi waliolazwa Taasisi ya Tiba ya Mifupa (MOI), jana wamepewa msaada wa dawa pamoja na mahitaji muhimu ya kibanadamu.

Msaada huo umetolewa na Kampuni ya simu ya Halotel na wafanyakazi katika kuadhimisha miaka sita ya kampuni hiyo ya utoaji wa huduma za mawasiliano.

Wafayakazi wa kampuni hiyo, walitembelea watoto hao na wazazi/walezi wao waliolazwa katika taasisi hiyo.

Mahitaji hayo ni pamoja na dawa na mahitaji muhimu ya kibinadamu, ambayo yatawawezesha watoto hao wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi kuimarisha afya zao, wanapokuwa wodini wakisubiri kupatiwa matibabu kwa njia ya upasuaji.

Akizungumza wakati wa kukabidhi mahitaji hayo, Naibu Mkurugenzi wa Halotel, Thang Bui Van akiwa na Ofisa Uhusiano wa nje Halotel, Yassir Matsawily, alisema katika kuhakikisha wanasaidia sekta ya afya nchini, wameona ni vyema kuendeleza fursa hiyo ya kuwatembelea watoto hao na kusherehekea nao kwa kuwapa msaada hiyo ya kijamii, ili waweze kuimarika kiafya wanapoendelea kupata matibabu wodini hapo na kuonesha upendo kwao na kutambua thamani yao katika jamii.

"Tunatambua changamoto mbalimbali, ambazo ziko katika kuwapa matibabu watoto wenye matatizo ya kiafya ya vichwa vikubwa na mgongo wazi wawapo wodini wakisubiri kupata matibabu ya upasuaji, hivyo katika kujali na kutambua thamani ya afya zao tumeona ni vyema tukawaletea mahitaji haya muhimu ya kuimarisha afya zao aliongeza Yassir," alisema.

Akiongea baada ya kukabidhiwa msaada huo kwa niaba ya wazazi wengine wodini hapo, Rose Vincent alisema, "Tunajisikia furaha sana kukumbukwa na kampuni ya simu Halotel na kupokea msaada huu kutoka kwao, tumefarijika sana na tunaomba waendelee na moyo huu huu wa kuisaidia jamii ya Watanzania."

Kwa upande wa uongozi wa MOI, Ofisa Uhusiano, Patric Mvungi alisema wamefarijika kupokea msaada huo kutoka Kampuni ya Halotel wanawashukuru kwa kuthamini afya za watoto hawa, pia kwa kuunga mkono jitihada za kuisaidia sekta ya afya nchini.

Alisema hiyo ni hatua mpya na kubwa na imekuwa endelevu katika kuimarisha ushirikiano na kampuni hiyo katika kuboresha sekta ya afya kwa ujumla."

Kampuni ya Halotel imekuwa ikijihusisha na kutoa misaada mbalimbali kwa jamii katika kuonesha inavyothamini na kujali katika nyanja mbalimbali, ikiwamo kuboresha sekta ya afya na elimu kama moja ya kipaumbele cha kampuni kwa maendeleo ya nchi.

# RC awaita wasomi awape ajira

**Na Richard Makore,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, amewaomba wasomi wote wenye shahada waliopo mkoani humo, kufika ofisini kwake awasaidie kupata mafunzo na mitaji, ili wajiajiri katika sekta mbalimbali, ikiwamo ufugaji wa samaki wa vizimba.

Gabriel alitoa ombi hilo kwa wasomi hao wakati akifungua kikao kazi cha Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB), kilichofanyika jijini hapa jana.

Alisema vijana wote wenye elimu ya juu kupitia mpango maalum atawasaidia kupata mafunzo ya ujasiriamali, mitaji na masoko, kwa ajili ya bidhaa watakazozalisha.

"Ufugaji wa samaki katika Ziwa Victoria hauhitaji kujenga mabwawa, bali wanafugwa kutumia vizimba na kuweka vifaranga vya samaki na mtu anapata mazao bora na mengi," alisema.

Alisema Mkoa wa Mwanza una vijana wengi wasomi, ambao hawana kazi za kuwaingizia kipato na kwamba yeye amejitoa kuwa mwalimu na mtu wa kuwaelekeza namna ya kufanya.

Akizungumza masuala ya mikopo kwa vyuo vikuu hapa nchini, Gabriel alisema, kiwango cha mikopo kimeongezeka kutoka Sh. bilioni 464 kwa mwaka 2020/21 hadi kufikia Sh. bilioni 570 kwa mwaka 2021/22.

Aidha, alisema idadi ya wanafunzi walionufaika na mikopo hiyo kwa mwaka imeongezeka kutoka 149,378 mwaka 2020/2021 hadi kufikia 162,000 mwaka 2021/2022.

Alisema anatamani kuona siku moja Mkoa wa Mwanza unakuwa wa wabunifu katika nyanja mbalimbali, ili kutoa fursa kwa vijana na watu wengine kupata kipato.

Alisifu HESLB kwa kuendelea kutoa huduma bora jambo ambalo limechangia kumaliza migogoro ya wanafunzi katika vyuo vikuu mbalimbali.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq-Badru alisema lengo la kikao hicho kilichowakutanisha maofisa mikopo kutoka vyuo vikuu vyote hapa nchini ni kuangalia masuala ya utendaji kazi.

Alisema vyuo na taasisi zinazotoa elimu ya juu zipatazo 130, maofisa mikopo wote katika vyuo hivyo wameitwa, ili kujadiliana na HESLB, ili kujua matatizo mbalimbali waliyokutana nayo mwaka ulioisha na kujipanga, kwa ajili ya mwaka ujao wa masomo.

Alisema ili kuwabaini wanafunzi wenye uhitaji wa mikopo ya elimu ya juu, HESLB imeingia makubaliano na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), ili wanafunzi wanaotoka familia masikini zinazofadhiliwa na mfuko waweze kupata mikopo.

Kupitia mpango huo wanafunzi ambao kaya zao zinafadhiliwa na TASAF watapata mikopo, wakiwamo yatima, mahitaji maalum na wenye ulemavu.

Alisema kipaumbele ni kwa familia maskini na kwamba kupitia TASAF, watahakikisha wanapata taarifa sahihi za wanafunzi walioomba mikopo ya elimu ya juu.

Kuhusu urejeshwaji wa mikopo kwa wanufaika, Babru alisema kwa mwaka jana walipokea marejesho ya Sh. bilioni 15 na mwaka huu yameongezeka na kufikia Sh. bilioni 18.



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni ya Enterprise Finance Ltd (EFL), Prof. Goodluck Urasa (kushoto), akizungumza na wafanyakazi, jijini Arusha hivi karibuni, wakati wa uzinduzi wa utaratibu wa kusherehekea mwezi wa huduma kwa wateja wa kampuni hiyo, ambao uadhimishwa mwezi Oktoba kila mwaka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# EFL yaanzisha mwezi huduma kwa wateja

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Enterprise Finance Limited (EFL), inayojishughulisha na huduma za fedha kwa wafanyabiashara na wafanyakazi, imezindua utaratibu wa kusherehekea mwezi wa huduma kwa wateja itakayofanyika Oktoba kila mwaka.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Prof. Goodluck Urassa, utaratibu huo ni mpya na kwamba una lengo la kukamilisha shughuli mbalimbali ilizokusudia kufanya katika kuboresha huduma zake.

Lengo lingine ni kuboresha huduma kwa wateja kila siku, utaratibu utakaowezesha menejimenti na wafanyakazi kushirikiana kujenga utamaduni wa kuwahudumia wateja kwa weledi na ubora wa hali ya juu kwa mwezi.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa EFL, Jacqueline Lujuo, alisema EFL imejipanga kuboresha uhusiano na wateja kwa kutoa huduma za ziada na kwamba wameweka utaratibu wa kuwatembelea kujua mahitaji yao, kusikiliza changamoto, kutoa ushauri wa kibiashara kwa wateja na jamii, kutoa mafunzo ya ujasiriamali na usimamizi wa fedha kwa wajasiriamali wanaopenda kushiriki na kujenga uwezo wa wafanyakazi kuwahudumia wateja kwa ufanisi.

Pia alisema EFL itajihusisha na shughuli za kijamii ikiwa ni pamoja na kuandaa michezo mbalimbali kati yake na taasisi nyingine ili kuchangia katika kuimarisha afya za wafanyakazi, wateja na jamii.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti huyo, taasisi hiyo imekusudia kuhakikisha kila mteja au mjasiriamali anayehudumiwa anajengewa uwezo wa kukua kibiashara.

"Mafunzo haya yalilenga kuwawezesha washiriki kuibua fursa za kijasiriamali, kusimamia biashara, kusimamia fedha na kujenga tabia ya uwajibikaji pia tunaendelea kutoa ushauri na mafunzo zaidi kupitia mitandao ya kijamii na vyombo vya habari na imeishauri jamii kufuatilia vipindi vyake," alifafanua.

Mmoja wa washirikia hao, Getruda Laizer, aliishukuru taasisi hiyo kwa mikopo nafuu iliyowawezesha kukuza biashara zao.

Naye Godfrey Massawe ambaye ni mkandarasi, alisema EFL imekuwa mkombozi wao kwa kuwapatia mikopo kwa wakati kwa ajili ya kutekeleza miradi.

Meneja wa EFL, Tawi la Arusha, Hekima Adam, alisema kampuni imejipanga kuwafikia wafanyakazi na wajasiriamali wote Kanda ya Kaskazini.

# TAKUKURU kumulika miradi ya kimkakati

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imeagizwa kufanya ukaguzi wa kina wa miradi yote ya kimkakati huku ikitakiwa ndani ya wiki mbili kuwasilisha taarifa ya kiuchunguzi ya ubadhirifu wa zaidi Sh. milioni 750 uliofanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, mkoani Mwanza.

Aidha, maofisa TAKUKURU wilaya nchini wameagizwa kufuatilia taarifa zote za kila mlengwa aliyekusudiwa na asiyekusudiwa ambaye ameingizwa kwenye Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF), ili serikali iwachukulie hatua watendaji waliotengeneza mipango na kuingiza wasio na vigezo vya kunufaika na mpango huo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye ziara aliyoifanya hivi karibuni mikoa ya Mwanza, Mara na Simiyu.

Aliagiza taasisi hiyo kuwachukulia hatua kwa watendaji na watumishi wa umma wanaoshiriki kwenye vitendo viovu vinavyohujumu utekelezaji wa miradi mbalimbali.

"TAKUKURU ngazi zote wafuatilie kwa kina kabisa miradi yote ya kimkakati, taarifa zote zinazotolewa na watoa taarifa kupitia namba yetu ambayo tunaitaja mara kwa mara 113, ili tufuatilie utekelezaji wa miradi."

"Yapo maeneo katika halmashauri nilizopita na kujionea fedha nyingi za miradi zimetolewa, lakini utekelezaji umekuwa ni mdogo, kwa mfano kule Sengerema tumejionea matumizi makubwa ya fedha na mradi wetu wa jengo la halmashauri haujafikia hatua yoyote," alisema.

"Niwaagize TAKUKURU ndani ya wiki mbili ofisi yangu ipate taarifa ya kiuchunguzi kuhusu ubadhirifu wa fedha zaidi ya Sh. bilioni 750 ambao umefanywa katika halmashauri kule Sengerema, na wahusika wote bila kujali nafasi zao TAKUKURU ichukue hatua, na sisi wizara tutachukua hatua kutokana na taarifa tutakazoletewa," alisema.

Alisema vitendo hivyo vinasababisha ubadhirifu wa fedha za umma na kuagiza TAKUKURU ngazi zote kufuatilia kwa kina miradi yote ya kimkakati.

Aidha, Waziri Mchengerwa alisema katika ziara yake alibaini baadhi ya watendaji kugawana asilimia 40 ya fedha za miradi kama posho ya kusimamia miradi ya kimkakati inayotekelezwa kwenye maeneo yao.

Akizungumzia kuhusu TASAF, alisema kwenye ziara hiyo kero zilizoibuliwa na baadhi ya walengwa kulalamikia kutotambuliwa na kuingizwa kwenye mpango huo kipindi cha kwanza, pili na tatu huku wengine wakilalamikia ucheleweshwaji wa malipo na kutofuata kalenda iliyowekwa.

"Nitoe maelekezo kuhusu TASAF, Halmashauri za Wilaya zote lazima zijiridhishe kwa kufuatilia malalamiko ya kaya ambazo hazikutambuliwa kwa kufanya uhakiki wa kaya zote ambazo hazikupata nafasi kutambuliwa na kuandikishwa (zilizoachwa) katika mazoezi ya utambuzi yaliyokamilika hivi karibuni kwenye vijiji, mitaa na Shehia zote ili kaya zote zenye sifa na zinazokidhi vigezo kuingizwa kwenye mpango," alisema.

Aliagiza TAKUKURU wilaya na mikoa kufuatilia na kujiridhisha na taarifa zenye ukinzani ili kupata taarifa sahihi na kutimiza malengo yaliyokusudiwa.

Aliagiza malipo ya kaya yafuate kalenda ya malipo na kutocheleweshwa ili kutumia vizuri ruzuku zao katika mahitaji ya msingi.

"Pia tathmini ya kina ifanyike ili kubaini changamoto za malipo kupitia njia ya mtandao kupatiwa suluhisho mapema na kwenye maeneo ambayo yana tatizo la mtandao walengwa walipwe kwa njia ya taslimu ili wapate kwa wakati," alisema.



Ofisa Mkuu wa Idara ya Fedha wa Benki ya Biashara ya DCB, Constantine Mtumbuka (katikati), Ofisa wa Magereza, Florian Rutha (kushoto) na Mhamasishaji wa Vikundi vya Kijamii, Asha Pembe, wakikata keki kuadhimisha Wiki ya Huduma kwa Wateja wa benki hiyo, katika Tawi la DCB Ukonga, jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tigo, Samsung wazindua simu mpya kisasa

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Tigo kwa kushirikiana na Samsung Electronics wamezindua simu janja aina ya Samsung Galaxy Z Fold3 na ZFlip3.

Ushirikiano huo ni sehemu ya mkakati wa Tigo wa kuongeza matumizi ya mtandao wa 4G na kuchangia ukuaji wa teknolojia ya kidigitali nchini. Mkuu wa kitengo cha maduka na bidhaa za intaneti wa Tigo, Mkumbo Myonga, akizungumza wakati wa uzinduzi wa simu hiyo, alisema: "Ni jambo kubwa sana kwetu kuchaguliwa na Samsung kuwa wa kwanza kuzihifadhi na kuuza simu za Samsung Galaxy Z Fold3 na ZFlip3 kwenye soko la Tanzania. Hii inaonyesha imani yao kwetu juu ya chaneli kubwa za usambazaji tulizonazo na pia kupitia timu yetu ya huduma kwa wateja inayotoa huduma zenye ubora wa hali ya juu."

"Lengo letu ni kuchochea mageuzi ya kidigitali katika maisha ya watu hapa nchini na ndio maana tumeungana na Samsung ili kuongeza idadi ya umiliki wa simu janja pamoja na matumizi ya data ili kuhakikisha watu wengi zaidi wanafikiwa na teknolojia hii," alisema Muyonga.

Muyonga aliongeza kuwa walenga kuongeza uenezaji wa simu janja nchini huku wakihakikisha wateja wao wanafurahia huduma za kidigitali kupitia mtandao mkubwa wa 4G hapa nchini. Na ndio maana wanatoa 96 Gb za intaneti kwa mwaka mzima kwa wateja wote watakaonununa Samsung Galaxy Z Fold3 na ZFlip3.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Meneja wa Samsung Tanzania, Suleiman Mohamed alisema Samsung imezindua simu ya Samsung Galaxy Z Fold3 na ZFlip3 toleo jipya ulimwenguni ya simu janja zinazojipinda ambayo itabadilisha namna ambavyo watu wanavyoishi na kuufurahia ulimwengu.

"Kuna mabadiliko makubwa kwenye sekta ya mawasiliano na namna watu wanavyo ujua na kuufurahia ulimwengu. Samsung inahakikisha inatoa teknolojia na vifaa vya kisasa zaidi ili kuendana na mabadiliko hayo. Kwa kutumia camera yenye mfumo wa AI unaweza kupata kila tukio na kuungana na uwapendao bila mipaka," alisema Mohamed.

# Exim yajadili fursa na wateja

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Exim Tanzania, imekutana na wateja wake mkoani Iringa pamoja na mambo mengine kujadili fursa za kibiashara.

Ilikutana na wateja hao mwishoni mwa wiki katika hafla ya chakula maalum kwa ajili ya wateja wake mkoani Iringa, ili kujadili fursa za kibiashara, mipango ya ukuaji na huduma zitolewazo na benki hiyo katika mkoa huo.

Akizungumza kwenye hafla hiyo iliyohudhuliwa na wadau mbalimbali wa benki hiyo wakiwamo viongozi wa kiserikali, wafanyabiashara wakubwa na wadogo pamoja na wafanyakazi wa benki hiyo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa benki hiyo, Jaffari Matundu, alisema, kupitia hafla hiyo walilenga pia kutoa fursa miongoni mwa wateja hao ili kufahamiana na kufungua wigo wa kufanya biashara pamoja.

"Pamoja na kushukuru kwa namna ambayo wateja wetu wamekuwa nasi hadi kufikia mafanikio ya ukuaji na ubora wa huduma zetu, hafla hii inatoa fursa kwa wateja wetu pia kufahamiana wao kwa wao na hivyo kufungua milango ya fursa baina yao," alisema Matundu.

Alisema hali ya uchumi katika mkoa huo inatoa fursa kubwa ya ukuaji kwa benki hiyo na hiyo ndio sababu imejipanga kuhudumia wateja wakubwa, wadogo na wa kati ili kuleta ustawi kwenye sekta muhimu kwa mkoa huo ikiwemo biashara, kilimo na ufugaji.

"Takwimu zinaonyesha Mkoa wa Iringa umeendelea kujenga uchumi imara na endelevu, na hivyo ufanisi katika mfumo wa fedha ni moja ya mahitaji ya muhimu na ya msingi katika ukuaji wa uchumi na maendeleo kwa ujumla. Benki ya Exim tumejipanga kuhakikisha tunafanikisha hilo pamoja," alisema.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Iringa, Ephraim Kyando, aliuomba uongozi wa benki hiyo kuangalia namna kujitanua zaidi mkoani humo kwa kuongeza matawi zaidi kwenye wilaya mbalimbali za mkoa huo ili huduma zake ziweze kuwanufaisha wananchi wengi wa mkoa huo.

# H'shauri zatakiwa kuchangamkia fedha za miradi

**Na Faustine Feliciane,** ALIYEKUWA KAHAMA

HALMASHAURI za wilaya zinazozunguka mgodi wa Bulyanhulu mjini Kahama zimetakiwa kuandaa miradi yenye manufaa, kwa ajili ya kufadhiliwa na mgodi wa Barrick unaomilikiwa kwa pamoja na serikali kupitia kampuni ya Twiga Minerals Corporation Limited.

Rai hiyo ilitolewa hivi karibuni na Naibu Waziri wa Madini, Prof. Shukurani Manya, wakati wa kikao na uongozi wa kampuni ya Barrick chini ya Mkurugenzi Mtendaji Mkuu, Mark Bristow na waandishi wa habari.

Alisema Kampuni ya Barrick ipo tayari kuwekeza kwenye maeneo yanayozunguka mgodi huo, lakini kwa kufuata sheria na utaratibu walizojiwekea.

"Pamoja na kuandaa miradi hiyo ni lazima nidhamu ya matumizi ya pesa iwepo, hakuna mtu au kampuni inayopenda kutoa pesa zake halafu wasione matunda ya pesa hizo ni lazima hiyo miradi itakayopitishwa isimamiwe kikamilifu na kuhakikisha kila pesa inaenda kufanya kazi iliyokusudiwa," alisema Prof. Manya.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa Barrick, Bristow, alisema kampuni hiyo itaendelea kushirikiana na jamii inayozunguka migodi yake katika shughuli mbalimbali za maendeleo.

Alisema Barrick imeanza mchakato wa kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Kahama Bulyanhulu, kwa ajili ya kuwezesha huduma za usafiri kwa wananchi.



ALHAMISI OKTOBA 14, 2021


# MIAKA 22 TAIFA BILA NYERERE



Ukurasa 14

Moringe, mjukuu wake Baba wa Taifa ayakumbuka makonzi yalimwadabisha





Ukurasa 12

**John Mwakangale: Swahiba wa Nyerere na mwenyeji wa Mandela Mbeya, 1962**

## MARAFIKI ZAKE 'DAMUDAMU'

# Kazini Rashid Kawawa na nyumbani mpinzani wa bao, Mzee Nyang'ombe

**Na Peter Orwa**

NAAM, kilele cha miongo miwili na ushee kifo cha Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, kila mahali ni maadhimisho ya kitaifa.


Ni wiki hiyo yote kuna mengi yanazungumzwa kuhusu maisha yake na miaka mingi ameendelea kujadiliwa kuhusu maisha yake.

Nyerere amekuwa na wasifu mmoja kwamba, licha ya kuwa na wadhifa wa juu kimataifa, lakini marafiki na mfumo wake maisha amekuwa akiishi wa kawaida zaidi. Eneo mojawapo ni marafiki aliyokuwa nao.

Kimsingi, falsafa na maisha yake binfasi yaliangukia kwenye itikadi ya Ujamaa na falsafa yake ya kuishi katika hulka ya Kiafrika na kupenda haki. Historia ya maisha yake inaonyesha hakuwahi kutoka nje ya mstari huo.

Kama binadamu yeyote, alikuwa na marafiki alioshirikiana nao. Katika mtazamo wa tafsiri ya maisha yake marafiki wengi waliangukia maisha ya kawaida mno, katika makundi makuu matatu: Ofisini na kisiasa: aliyoishi nao nyumbani; na kutoka jumuiya mbalimbali za kijamii kama vile makanisani.

Historia yake mwalimu inamwonyesha katika kila kundi la marafiki, aliishi nao kwa namna yao, kadri ya mahitaji yalivyokuwapo.



Rais Julius Nyerere (kulia) alipoongozana na viongozi wenzake wa awamu ya kwanza, akiwamo Waziri Mkuu, Rashid Mkuu Rashid Kawawa, (watatu kutoka kulia). **PICHA: MTANDAO**

Kuna jambo la kipekee jamii nyingi zikiwamo waliokuwa watoto tangu zama hizo walidiriki kufananisha urafiki kwa mfano wa 'Nyerere na (Rashidi) Kawawa.'

Hata ikakumbukwa, kuna wakati Mwalimu Nyerere, alipopewa kauli ambayo hakufurahia kutoka kwa mwanasiasa wa upinzani, dhidi yake na Kawawa, alionyesha kugadhabika akitishia kumshtaki kwamba kilichomuudhi sana ni hatua kumdhihaki Rashidi, kwa maana ya Kawawa ilimkera sana, huku kejeli kwake aliziita 'ni upuuzi tu'.

Ni jambo lililozua swali kubwa kutoka kwa umma, ni kiasi gani anamthamini Mzee Kawawa ambaye haijawahi kutokea historia yake ya madarakani zaidi ya miaka 30 kabla na baada ya uhuru, ndani ya TANU na serikali hawakukwazana.

Mwandishi wa makala katika faragha na Mzee Kawawa nyumbani kwake Madale, Dar es Salaam, muda mfupi baada ya kifo cha Baba wa Taifa, kwanza hakuficha urafiki wao wa 'damudamu.'

Kawawa anasema binafsi aliguswa na Nyerere akiwa Mwalimu na yeye mwanafunzi, pale Baba wa Taifa alipoandamana na mwalimu mwenzake (Balozi) Tibandebage kusimamia mjadala wa wanafunzi (debate).

Kawawa anasema, alikoshwa na stadi zao za lugha na hasa kutoka kwa Nyerere, kuanzia sauti, ubora wa lugha na alivyojenga hoja zake, bila Nyerere kujua.

Baada ya kuhitimu masomo, Kawawa alijikita katika harakati za haki za wafanyakazi akiwa katika iliyokuwa Shirikishi la Wafanyakazi wakati huo TFL. Kazi nzuri ya kuitikisa serikali ya mkoloni nayo ikamgusa Mwalimu Nyerere wakati huo mwaka 1955 akiwa amejikita katika harakati za TANU.

Nyerere aliiomba faragha naye washirikiane katika harakati na daima waliungana kuwa maswahiba wa kikazi hadi majumbani hadi kuzikana.

Palishuhudiwa hata kimataifa, hasa katika zama za miaka ya 1970, Tanzania ikiwa na urafiki wa juu na China wakati Nyerere alikuwa karibu sana na Rais Mao Tse Tung, Kawawa alikuwa sambamba na Waziri Mkuu mwenzake, Chuo Enlai, hata wakafika kuvaa aina ya mashati waliopenda yasiyo na kola, maarufu 'Chuoenlai.'

**INAENDELEA UK.13**

# John Mwakangale: Swahiba wa N na mwenyeji wa Mandela Mbeya

**Na Mwandishi Wetu**

• Waliiva ujana wa PAFMECA, TANU hadi uzeeni • Walifuatan Mugabe kwa kupata uhuru • Alitekeleza Azimio Arusha kwa K



John Mwakangale, akihutubia mkutano wa hadhara wa TANU wilayani Rungwe mkoani Mbeya. Kushoto kwake walioketi ni Mwenyekiti wa T Julius Nyerere, akiwa pamoja na wanachama wengine wa chama hicho waliohudhuria mkutano huo. **PICHA ZOTE: JBM MAKTABA**

UNAPOZUNGUMZIA uhuru wa Tanganyika, hukosi kutaja baadhi ya majina ya waliokuwa begabega na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Hapo ndipo unapokutana na mojawapo, mwaharakati wa nchini na Afrika, aliyekuwamo katika orodha ya kumuunga mkono, John Benedict Mugogo Mwakangale.

Marehemu Mzee Mwakangale kama alivyozoea kujiita JBM, kwa kumaanisha ufupisho wa jina lake, ambalo aliitumia zaidi kama ufupisho na alama ya saini yake binafsi.

Wakati leo anakumbukwa Mwalimu Nyerere tangu kifo chake kutimia miaka 22, John Mwakangale anatimiza miaka 19, tangu alipofariki nyumbani kwake Nditu wilayani Rungwe, mkoani Mbeya,

Ni utangulizi wa dodoso la gazeti Nipashe, lilipongumza na mtoto wa marehemu John Mwakangale, ambaye sasa naye ni Mzee Stephen Mwakangale, nyumbani kwake Forest jijini Mbeya, namna baba yake alivyoishi kisiasa kwa uswahiba mkubwa kikazi na binafsi na Mwalimu Nyerere.

Pia, ndiye aliyekutana na kuwa mwenyeji wa shujaa na Rais wa Afrika Kusini, Nelson Mandela, hata wanasiasa wengine wa Afrika.

Mandela, kwenye kitabu chake kiitwacho 'LONG WALK to FREEDOM' amemwelezea John Mwakangale na namna alivyompokea mkoani Mbeya mwaka 1962, kabla ya kwenda Addis Ababa, Ethiopia kushiriki Mkutano wa Muungano wa Ukombozi Kusini na Mashariki mwa Afrika (PAFMECA).

Mazungumzo ya mwandishi wa Nipashe na mtoto huyo wa marehemu Mwakangale, Mzee Stephen, ana ufafanuzi kuhusu aliyohadithiwa na mazungumzo yao ya maswali na majibu. Fuatilia mazungumzo yao ya 'ana kwa ana':

**Mwandishi: Unamtaja vipi Mzee Mwakangale katika siasa za Tanzania, kiserikali na wakati huo chama cha TANU, alikuwa nani?**

**Stephen:** Kabla ya uhuru, baba alikuwa mwajiriwa na mwanataaluma katika mifugo, yaani daktari wa mifugo, ilikuwa fani yake. Baadaye aliamua kujikita na siasa na mwaka 1956 akajiunga na Tanganyika African National Union (TANU), akishika nafasi ya Katibu wa Mkoa (Mbeya).

TANU ilipozaliwa, kulikuwapo na wakereketwa wengi kisiasa akiwamo baba, Nyerere, Joseph Kizurira Nyerere (mdogo wa Baba wa Taifa), (Kanali Mohamed) Kissoky na wengine wengi ambao

> **Asubuhi yake tulitoka kuelekea Mbeya, mji wa Tanganyika uliopo mpakani mwa Kaskazini mwa Rhodesia (sasa Zimbabwe). Tukiwa juu angani rubani alijaribu kuwasiliana na Mbeya.**

walijikita katika ukombozi hata Kusini mwa barani Afrika.

Alikuwa PAFMECA akishiriki harakati za ukombozi Kusini mwa Afrika. TANU ilipoasisiwa alichaguliwa na kuonyesha mchango mkubwa kisiasa na harakati hizo ilimfanya kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Kutunga Sheria (LEGCO) mwaka 1957.

**Mwandishi: Mahsusi ukienda katika uhusiano wake na Nyerere, yepi unaweza kuyaorodhesha alivyotoa mchango wake kwa mwalimu na serikali yake, maana ni vigumu kutofautisha TANU, Nyerere na serikali yake?**

**Stephen:** Uhusiano unakuwapo, kwa sababu ya shughuli walizofanya ziliendana, siasa kuwa mwana TANU, pia Nyerere hivyo hivyo na baada ya uhuru wa Tanganyika, Nyerere akawa Rais wa Tanzania. Aliendelea kumteua kwenye nafasi za kitaifa na mkoa mara kadhaa, akijua atamwakilisha vyema kwa wananchi.

Mwaka 1962, alikuwa Mkuu wa Mkoa Nyanda za Juu Kusini na mwaka uliofuata, aliteuliwa na Rais kuwa Junior Minister of Local Government and Housing (Naibu Waziri wa Serikali ya Mitaa na Nyumba). Pia akawa Mkuu wa Mkoa Dodoma mwaka 1964.

**Mwandishi: Wewe ni mwanawe? Naamini unajua huku Mbeya walisema Nyerere alimtegemea sana Mwakangale kama mmoja wa watu wake muhimu. Unaelezeaje?**

**Stephen:** Mikutano kadhaa, baba aliandaa maeneo tofauti ya Mbeya. Nakummbuka ambao ulifanyika Tukuyu na Mwalimu Nyerere, alihudhurua, wakiwamo viongozi kadhaa wa TANU.

**Mwandishi: Je, kuna wengi waliokuwa kama Mwakangale hapa Mbeya, unawaelezeaje kabla na baada ya uhuru?**

**Stephen:** Alishirikiana na Mohammed Kissoky, Fatma Mwashambwa, Binti Matola. Kwa ujumla Kusini mwa Afrika nchi kadhaa zilikuja Tanzania kabla na baada uhuru na baba akiwa mwenyeji wao na baadhi walilala nyumbani mwetu Makandana, Tukuyu (Mbeya). Kulikuwa na 'cross borders' (njia ya mkato), Malawi, Zambia, Afrika Kusini kote huko.

**Mwandishi: Nyerere alipokuja Mbeya, unamkumbuka uhusiano wao ulivyokuwa?**

**Stephen:** Nakumbuka waliishi vizuri hadi mwisho, marafiki wa kweli tangu ujana wao. Nakumbuka mwaka 1967 nikiwa likizo nikisoma chuoni Nairobi, baba akaniambia anatakiwa kuuza sehemu yake, nikamjibu "ikiwa kutoka moyoni unakubaliana na hilo na Azimio la Arusha, uza" na kweli akauza. Kwa hiyo alikuwa mkweli.

Kimsingi, alikuwa muwazi, mkali na msimamo. Alisimamia alichokiamini. Ndio maana walielewana na Nyerere na alimwamini.

**Mwandishi: Ukimkumbuka baba yako, unadhani ni mambo yepi katika maisha yake binafsi na hata kisiasa wamefanana sana na picha ya Nyerere?**

**Stephen:** Wanaweza kufanana kwa kile walichotaka kifanikiwe, ndio maana walielewana na kuwa kati ya marafiki wake wakubwa.

**Mwandishi: Je, mama yenu alikuwa mwanasiasa au kuambukizwa na baba yako ule U-Nyerere?**

**Stephen:** Mama hakuwahi kuwa mwanasiasa.

**Mwandishi: Kumbuka matukio muhimu ya nchini, uhuru wa Tanganyika mwaka 1961, Tanzania ya chama kimoja, kisha Muungano wa mwaka 1964; Azimio la Arusha 1967; Azimio la Iringa mwaka 1972, Siasa ni Kilimo; na Azimio la Musoma, Siasa ni Elimu, pia mwaka 1974 kuanzishwa vijiji vya Ujamaa mwaka 1975 na**

# lyerere , 1962

## a kumpongeza kuuza shamba



ANU,

**kuzaliwa CCM (mwaka 1977), baba alivyoenda 'kumsapoti' Nyerere au baba kuadhimisha uhuru?**

**Stephen:** Matukio kadhaa tumeyakuta hasa katika picha, kwa sababu kabla ya uhuru nilikuwa masomoni shule za bweni kwa muda mrefu. Pia, chuo kikuu nje ya nchi na baada ya uhuru, nilikuwa nafanya kazi mikoa tofauti.

Hivyo, nilijua baba alikuwa akifanya shughuli mbalimbali za chama na serikali, hata kama sikushuhudia ana kwa ana.

Pia, iwapo alikuwa mkoa fulani nilipokuwa nikifanyia kazi, nilifahamu zilikuwa shughuli zake za kichama na alifika nyumbani kutusalimia.

**Mwandishi: Nasikia alikuwa mjamaa. Elezea alivyokuwa, mlo na mavazi yake?**

**Stephen:** Mavazi alikuwa anavaa mchanganyiko suti ilikuwa vazi rasmi. Ila alivaa zaidi kaunda suti na zile kama za Mao (Chuoenlai), ni kama wote walikuwa na msimamo mmoja katika mavazi.

### URAFIKI NA MANDELA

Kwenye kitabu chake, 'LONG WALK for FREEDOM', Shujaa wa siasa za Afrika Kusini Nelson Mandela katika sehemu ya kurasa za kitabu hicho, anaeleza namna alivyokwa Mbeya, akipokewa na mwenyeji wake, John Mwakangale mwaka 1962. Sehemu ya nukuu yake Mandela katika kitabu hicho, ni kwamba:

"Asubuhi yake tulitoka kuelekea Mbeya, mji wa Tanganyika uliopo mpakani mwa Kaskazini mwa Rhodesia (sasa Zimbabwe). Tukiwa juu angani rubani alijaribu kuwasiliana na Mbeya. Mbeya... Mbeya, Lakini hakujibiwa!

"Hali ya hewa haikuwa nzuri, mawingu...hatimaye anga likawa safi...tulifanya 'booking' kwenye hoteli ya kawaida (Mbeya Hotel) na kukuta umati wa Waafrika, Wazungu hasa katika varanda (barazani), wakiendelea na mazungumzo yao taratibu.

"Tulikuwa tukimsubiri Mr. Mwakangale wa Chama cha Tanganyika African National Union (yaani TANU), mbunge na bila ya kujua kwamba alikuwa amewasili (hotelini). Alikuwa akitutafuta..."

Pia, mwaka 1990 wakati Nelson Mandela alipozuru Tanzania mara baada ya kutoka kifungoni, alipowasili Dar es Salaam, John Mwakangale alikuwa miongoni mwa wageni wa kitaifa walioalikwa kumlaki Mandela, akiwa Rais wa Afrika Kusini ambaye aliiongoza taifa lake kwa muhula mmoja tu.

Kadhalika, mwaka 1999 wakati Nelson Mandela alipofika kuwaaga Watanzania mkoani Dar es Salaam, kati ya wageni waalikwa, Mandela aliomba awe na orodha ya wageni wake maalumu siku hiyo na kukutana nao kwenye hafla ya kumuaga, akiwamo John Mwakangale, akipewa mwaliko huo na mwanaharakati huyo akifahamika zaidi kama 'Madiba' kutoka Afrika Kusini, aliyeacha historia na alama kubwa ya ukombozi duniani.

Pia John Mwakangale alisafiri na ujumbe wa Rais Nyerere hadi Zimbabwe, wakati huo ikiongozwa na Rais Reverend Banana huku Robert Mugabe akiwa, Waziri Mkuu, muda mfupi baada ya kupata uhuru Aprili 1980.

### KIFO CHAKE

Mnamo Januari mwaka 2002, John Mwakangale, alifariki dunia nyumbani kwake Nditu, wilayani Rungwe, ikiwa ni miaka mitatu na miezi mitatu tangu kifo cha rafikiye, Mwalimu Nyerere.

Ni tukio lililomgusa aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tatu, Hayati Benjamin Mkapa, aliyetuma salamu za rambirambi na barua kwa familia kuwafariji.

Kijijini Nditu ni umbali zaidi ya kilomita 10 kutoka Katumba, eneo la umbali mfupi kutoka Tukuyu mjini, penye barabara inayoelekea Mashariki maeneo kama Mwakaleli na Lwangwa, ambako sasa ni Wilaya ya Busokelo. Pia, pana umbali mfupi kuelekea kijiji jirani cha Suma anakotokea, Profesa Mark Mwandosya.

Mkoa umemheshimu kwa siasa zake hapo na kitaifa, ambako jijini Mbeya kumetengwa viwanja maalum vilivyobeba jina lake - Viwanja vya John Mwakangale.

> **"Tulikuwa tukimsubiri Mr. Mwakangale wa Chama cha Tanganyika African National Union (yaani TANU), mbunge na bila ya kujua kwamba alikuwa amewasili (hotelini).**



John Mwakangale, akizungumza na wanawake wa UWT. Kushoto kwake ni Mama Maria Nyerere na kulia kwake ni Fatma Karume.

# Kazini Rashid Kawawa na nyumbani mpinzani wa bao

INATOKA UK.11

Mjane wa Mwalimu Nyerere, anaifafanulia Nipashe kijijini Butiama mwaka mmoja baada ya kukutana na Kawawa, akisema hata kuwa watoto wengi kutoka familia ya Kawawa kufika katika maziko ya Baba wa Taifa kijijini Butiama, ni kwamba walimtafsiri ni baba yao, kwa maana ya uhusiano wa karibu kifamilia na waliishawahi kuishi majirani.

### MZEE NYANG'OMBE

Unapofika kijijini Muryaza, umbali wa kilomita saba Kaskazini Mashariki ya Butiama, penye barabara kuu iendayo Ikizu kutoka Nyamuswa, alikuwapo Mzee Nyangombe Warioba, ambaye sasa ni marehemu.

Akiwa na umri tofauti ya miaka saba mdogo kwa Nyerere, Mzee Nyango'mbe alitokea kuwa rafiki wa karibu mno wa Mwalimu Nyerere, tangu utoto wao na ukachukua wastani wa miaka 70.

Moja ya sifa za urafiki wao, ulikokuwa katika mchezo wa bao (soma ukurasa 14) wakibishana sana. Hata katika maisha yake, Mzee Nyang'ombe alimfahamu vyema Nyerere kitabia, mlo na hata kumuiga sauti kwa ufasaha, iwe katika hali ya tabasamu hata kukasirika, alikuwa mithili ya 'google' inayomhusu Nyerere.

Anasimulia kwamba, hata mara moja hawakuwahi kuweka urafiki wao katika siasa, lakini 'walishibana' na Mwalimu kuna wakati akimwandalia usafiri kutoka kijijini kwake hadi Dar es Salaam. Kwa mujibu wa Nyangombe, pindi alipofika Dar es Salaam alipatia heshima zote za mgeni rasmi wa kifamilia, akikaa Ikulu na Mwalimu katika makazi yake Msasani.

Hata hivyo, anasema kila ilipofika jioni, alituma usafiri kwenda Msasani ambako waliongea na kubishana katika mchezo mpaka usiku sana.

Anasimulia, licha ya Nyerere kumjengea nyumba kijijini kwake Muryaza, kazi walipewa Jeshi la Magereza baada ya kustaafu muda wote Nyerere alimhamisha rafiki yake huyo kukaa naye Butiama.

Alipata nafasi kurudi kwake Muryaza, pindi tu Mwalimu amesafiri na anapotua kijijini Butiama, alituma gari kumpeleka Butiama, ambako walichuana sana katika mchezo bao.

Pia lingine walikuwa na shamba la pamoja, walilima huku wakipeana michapo shambani wakarudi kula pamoja na mapumziko jioni wako wote katika bao.

Pia Nyang'ombe anamtaja mtumishi wa nyumbani Butiama, ambaye alikuwa kijana pia, alikuwa rafikiye mkubwa Mwalimu wa Katibu.

Anakumbuka hata wakati dakika chache kabla hajaanza safari ya kwenda kutibiwa Uingereza, Baba wa Taifa alimnong'oneza kuna jambo anataka kumwambia pindi angerudi tu, lakini halikutimia, alifariki.

# Moringe, mjukuu wake Baba wa Taifa ayakumbuka makonzi

- Penye shule, nidhamu alirejea ualimu
- Alihusudu bao, tusipokaa kimya konzi!

**Na Sabato Kasika**

KATIKA kuadhimisha kumbukumbu ya kifo cha Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere. Yapo mengi yanaendelea na jana huko Geita, kulikuwapo na mjadala maalum.

Watu wa kada mbalimbali wa wanazungumzia wanavyomfahamu Mwalimu Nyerere, miongoni mwao akiwa mjukuu wake, Moringe Magige Nyerere.

Mtu anapotamka tu jina la Moringe, ambalo ni nguzo nyingine ya taifa, marehemu Edward Moringe Sokoine, inaibua maswali.

Hapo ndipo mhusika analitolea ufafanuzi kwamba: "Watu wengi wamekuwa wakiuliza jina hili kwamba nilipewaje? Nilipewa kama kumbukumbu yake hasa baada ya kuondokewa na mmoja wa wasaidizi wake (Mwalimu Nyerere) wa karibu serikalini."

Moringe ambaye sasa ni mtu mzima na mtumishi wa umma, anaiambia Nipashe kuwa, alizaliwa miezi minne tangu kutokea kifo cha aliyekuwa Waziri Mkuu wa Tanzania, Hayati Moringe Sokoine, Aprili 12, mwaka 1984 huko Morogoro, kwa ajali ya gari.

Mjukuu huyo wa Baba wa Taifa, yuko wazi kuhusu hulka aliyoifahamu kutoka kwa babu yake kwamba 'ni kipenzi chake' na ndio sababu hakusita kumpatia zawadi ya jina hilo mzaliwa huyo wa Monduli, abaki kuwa kumbukumbu ya kudumu ndani ya familia ya Nyerere.



Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere (wapili kulia) akicheza bao, enzi ya uhai wake. **PICHA: MTANDAO**

### MAKONZI KWETU

Kwa sasa, Moringe anajitambulisha ni Ofisa Mwandamizi wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), jijini Dar es Salaam, akiwa na ufafanuzi namna babu yake alipenda kumwadhibu kwa 'makonzi' pale anapoenda kinyume katika nidhamu ya maisha nyumbani.

"Babu hakutulea vibaya, bali alipenda maendeleo yetu, ndiyo maana alitupiga makonzi pale tulipomkosea, hasa wajukuu ambao walikuwa na utundu wa kitoto, waliyapata kisawasawa," anasema Moringe.

Mjukuu huyo wa Baba wa Taifa, anasema babu yao alikuwa nao karibu kuhakikisha wanaepuka makundi yasiyofaa na kwamba anajigamba ndiyo malezi yamemfanya leo kuwa mtu mwema kwenye jamii.

"Kwa ujumla ni kwamba babu alitupenda na aliipenda familia yake, kwani pamoja na makonzi, tulikuwa tunakula naye chakula, pia wakati akiwa amepumzika tulikuwa tukimtania na kucheka naye," anasimulia.

> **Babu hakutulea vibaya, bali alipenda maendeleo yetu, ndiyo maana alitupiga makonzi pale tulipomkosea, hasa wajukuu ambao walikuwa na utundu wa kitoto, waliyapata kisawasawa.**



Mjukuu wa Baba wa Taifa, Moringe Magige Nyerere akiwa ofisini. **NA MPIGAPICHA WETU**

Moringe anasema baadhi ya wanaamini kuwa mababu huwapenda wajukuu hawawakanyi wanapofanya makosa, lakini Moringe anakana hilo lilikuwa kinyume kwa babu yake, nafasi ya msamaha kwa makosa haikuwapo, kuachiwa watakavyo.

### PENYE SHULE?

Kama ambavyo baadhi ya wazazi na walezi wanaojua umuhimu wa elimu hufuatilia maendeleo ya watoto wao shuleni, anasema Baba wa Taifa naye alifanya hivyo kwa wajukuu wake aliokuwa anaishi nao Butiama.

"Babu hakuwa na mzaha na elimu, alikuwa akifuatilia maendeleo yetu shuleni, kwani kila mwisho wa muhula alikuwa akitukusanya na kukagua matokeo ya kila mmoja wetu ili kujiridhisha kama tunafanya vizuri," anasema.

Mjukuu huyo anataja masomo ya Hisabati na Kiingereza kuwa ndiyo alikuwa akiwahimiza wayakazanie kwa kuwa ndiyo msingi mzuri wa kujua masomo mengine kirahisi kwa kuwa yako kwenye lugha ya Kiingereza.

"Kimsingi, alijua bila kuwa na msingi mzuri wa lugha ya Kiingereza, inakuwa vigumu kuyaelewa kwa ufasaha masomo mengine, ndiyo maana alitukazania na mimi nimeona umuhimu wa kile alichosisitiza," anasema.

Anafafanua kuwa pamoja na hayo, aliwafundisha kuhusu maisha ya kawaida mara baada ya kujitegemea, kwa kuepuka kujipatia mali kwa njia isiyo halali au kujionyesha kwa kuwa wanatoka kwenye familia hiyo maarufu nchini.

"Tunapoadhimisha kumbukumbu ya miaka 22 ya kifo cha Baba wa Taifa, binafsi ninamkumbuka kwa mengi aliyokuwa akifanya nyumbani, hasa baada ya kustaafu, kwani wakati wa uongozi wake nilikuwa sijazaliwa," anasema.

"Ukifuatilia historia ya babu utagundua kwamba hakuwa mtu wa kujilimbikizia zisizo za halali, hivyo hata watoto na wajukuu zake alitamani tuishi maisha kulingana na kile tunachokipata kihalali," anasema.

### UBISHI KWENYE BAO

Moringe anasema, babu yake alikuwa na rafiki binamu, aliyemtaja kwa jina la Nyang'ombe ambaye walikuwa wakicheza naye bao kila mara na hakutaka kuzongwa na mjukuu anapokuwa anacheza.

"Wakati akicheza bao na rafiki yake, sisi tukiwa wadogo tulikuwapo tunashuhudia, lakini hakutaka kuzongwa na wajukuu wakati anacheza, alitaka kuelekeza umakini kwenye bao ili asifungwe," anasema.

Anasema, kama ilitokea mtoto akakatiza na kusababisha ashindwe kuelekeza akili kwenye bao, alimpiga makonzi, na kwamba ilibidi wawe makini wasumsumbue anapokuwa kwenye mpambano wa bao.

"Yaani ukikatiza mbele yake wakati anacheza bao lazima upate konzi, kwani alitaka kama unashuhudia mechi yao, basi ukae utulie uone anavyopambana na Nyang'ombe hadi mwisho wa mchezo," anasema.

Anaongeza kuwa wakati mwingine Baba wa Taifa na rafiki yake walicheza hadi usiku hali ambayo iliwafanya (wajukuu) kuchoka kushindwa kuendelea kuwashuhudia na kuamua kwenda kulala.

Kwa mujibu wa Mzee Nyang'ombe Waribo katika simulizi yake miaka 20 iliyopita, kijijini kwake Muryaza umbali wa kilomita saba kutoka Butiama, Mwalimu Nyerere alikuwa mbishi katika mchezo huo na mbwembwe nyingi kumkosoa mpinzani wake, ambao ni marafiki tangu ututoni.

Anasema hakuwa tayari kwenda kulala, kuna wakati hadi saa sita usiku, hasa pale anapofungwa mchezoni, hata wanapoenda kupumzika, ananuia kurudiana siku inayofuata na inapotokea kafungwa siku hiyo, anaamua kesho yake kurudiana.

Nyang'ombe, ambaye sasa ni marehemu, ana simulizi kwamba inapotokea Mwalimu ana safari siku inayaofuata na ameshafungwa, wakati huo mara nyingi akitumikia kamati inayohusika na ukombozi Afrika, alinuia hata alipokanyaga tu kijijini Butiama, alituma gari kumfuata Nyang'ombe wapambane tena.

Ni ushindani ambao Nyang'ombe anauhadithia kuwa, Mwalimu Nyerere alitamba, hasa alipotoka safari akinukuu aliyomkejeli nayo kimchezo "nimetoka Lagos (Nigeria) unapajua wewe?" Anasema huku akifafanua kuwapo mbwembwe za kuwanunulia soda mashabiki waliojaa kutazama mpambano huo wa kijiji.





## Wadau watakiwa maoni kuboresha mfumo wa afya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WADAU wa sekta ya afya nchini wametakiwa kutoa mapendekezo kwa serikali namna ya kuboresha zaidi mfumo wa afya nchini ili Watanzania wapate huduma bora bila kumuacha mtu nyuma.

Ally Kebby, Meneja wa mradi wa HPSS-Tuimarishe Afya unaotekelezwa na Shirika la Swiss TPH kwa kushirikiana na serikali kuimarisha mfumo wa afya kupitia afua mbalimbali hususan Bima ya Afya ya CHF iliyoboreshwa, aliyasema hayo jana kwenye mkutano wa nane wa afya nchini linalofanyika jijini hapa kwa siku tatu.

Alisema mfumo wa afya unatakiwa kuwasaidia makundi yote nchini bila kumuacha mtu yeyote nyuma kutokana na serikali kuwekeza kwenye sekta ya afya kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita na sasa ikiwamo kujenga miundombinu na kuajiri watumishi.

"Kama mnavyosikia fedha nyingi zimelekezwa katika kuimarisha zaidi mfumo wa afya, kununua vifaa vya kisasa, magari ya kubebea wagonjwa, haya yote yanalenga kuwafikia wagonjwa bila kujali maeneo walipo," alisema.

Alisema mradi huo utakuwa na mawasilisho saba kwenye mkutano huo ambayo yamejielekeza kwenye bima ya afya, afya ya jamii na eneo la dawa.

"Eneo la dawa limekuwa lina changamoto nyingi upande wa ugavi, menejimenti kuna vitu vingi tumefanya na kutafiti tutawasilisha kwenye mkutano huu ili watu wengi wajifunze na sisi pia tutapokea kutoka kwa wengine," alisema.

Aidha, alisema CHF inahudumia wananchi wa kawaida na wale ambao wamejiajiri kwenye shughuli za kilimo, uvuvi, sekta rasmi na zisizo rasmi inawapa uhakika wa matibabu.

Vile vile, alisema katika ugavi na usimamizi wa dawa kwenye vituo na uboreshaji wa vifaa tiba kwa kuwa na mpango mzuri wa ununuzi, matengenezo kinga na ukarabati wa vifaa ambapo havifanyi kazi ili kutoa huduma bora.

"Eneo jingine ni uimarishaji wa afya ya jamii kwa kuboresha huduma za afya kinga kwa kuhakikisha wananchi wengi hawapati maambukizi hasa kwenye magonjwa yanayoepukika wananchi wajikinge nayo," alisema.

Alisema katika mkutano huo wataangalia matokeo ya utekelezaji kwa mwaka uliopita ili kuimarisha sekta ya afya.

Alifafanua kupitia mkutano huo yatatolewa mapendekezo na ushauri kwa serikali ili kuboresha zaidi mfumo wa afya bila kumuacha mtu nyuma wala kujali anaishi eneo gani.

# Mpango wa Afya ya jamii wapunguza vifo mama/mtoto

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa kitengo cha elimu ya afya Zanzibar, Halima Ali Khamis, amesema Mpango wa Afya Jamii unaotekelezwa visiwani humo umesaidia kuifikia jamii na kuchangia kwa kiasi kikubwa kupunguza vifo vya mama na mtoto.

Khamis, alibainisha hayo juzi jijini hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuwasilisha mada kwenye kongamano la nane la afya nchini (THS).

Alisema, mpango huo unaratibiwa kidijitali na umewezesha wananchi wengi kufikiwa na kupata huduma za afya za uhakika.

"Katika utekeleza mpango huu tunawatumia watoa huduma ngazi ya jamii ambao tumewafundisha masuala mbalimbali na wao wanapokwenda katika jamii kutoa huduma kupitia simu zao kila wanachokikuta wanatoa ripoti kwetu na sisi tunachukua hatua kwa haraka," alisema.

Pia alisema kutokana na kutumia simu hizo ambazo zimeunganishwa kutumia mfumo wa GIS, wataalamu wa afya wanaweza kufuatilia kila kitu kinachofanyika kupitia mfumo huo.

"Watoa huduma tunaowatumia ni kutoka katika jamii husika hivyo wanavyopita katika kaya na kutoa huduma za afya wakiona kuna shida fulani kama vile mtu anatakiwa kupata matibabu wanamwelekeza hivyo hali hii pia imesaidia kupunguza watu kwenda kwa waganga na kwenda kupata huduma sahihi za afya," alisema.

Vilevile, alisema watoa huduma hao wamesaidia kuongeza idadi ya kinamama ambao wanahudhuria kliniki mapema na kupunguza vifo vya wajawazito na watoto chini ya miaka mitano.

Kadhalika, alisema kuwa mpango huo umesaidia kufikisha elimu ya malezi na makuzi kwa wazazi wa maeneo mbalimbali Zanzibar.

"Awali kabla ya elimu ya makuzi na malezi kwa wazazi kulikuwa na changamoto kubwa ya ukuaji mbovu pamoja na matatizo ya utapiamlo uliokuwa ukisababishwa na wazazi wasio na elimu ya malezi na makuzi," alisema.

Alisema hadi sasa wamefundisha watoa huduma ngazi ya jamii 2,300 ambao wamesajili watu milioni 1.16 sawa na asilimia 73 ya wakazi wote wa Zanzibar ambao wamepatiwa huduma kupitia mpango huo.

"Watoa huduma ya afya hawa wameweza kukomesha pia vitendo vya unyanyapaa kwa wagonjwa ambao ulikuwa ukifanywa na wauguzi wa afya, lakini kutokana na wao kuwa sehemu ya jamii wamekuwa wakiwahudumia bila kuwanyanyapaa na kuwafanya wahudumu wa afya kubadilika," alisisitiza. Hata hivyo, aliiomba serikali kuona namna ya kuwawezesha watoa huduma hao ngazi ya jamii ili kuingizwa kwenye mfumo wa ajira rasmi.

"Hivi sasa wanapata posho kama Sh. 50,000 kwa mwezi hali ambayo inawalazimu wengine ambao tayari wameshapata mafunzo kuondoka kwenda kutafuta kazi nyingine hivyo tunalazimika kila mara kufundisha wengine wapya kuziba nafasi zao," alisema.



Mbunge wa Jimbo la Dodoma Mjini, Anthony Mavunde (mwenye kofia), akisaidiana na wananchi wa Kijiji cha Mkoyo, kujenga mmoja ya vyumba vya madarasa ya Shule ya Sekondari Mkoyo, nje kidogo ya Jiji la Dodoma juzi, baada ya kuchangia mifuko 100 ya saruji pamoja na matofali 200 kwa ajili ya ujenzi huo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kiwanda cha mbolea Itracom kupunguza bei

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, amesema ujenzi wa Kiwanda cha Mbolea cha Itracom unaoendelea katika eneo la Viwanda Nala, jijini hapa utasaidia kuondoa adha ya bei kubwa ya mbolea kwa wakulima nchini.

Prof. Mkumbo aliyasema hayo jana alipofanya ziara ya kutembelea na kukagua viwanda na miradi inayosimamiwa na wizara katika Mkoa wa Dodoma na kukagua ujenzi huo, eneo la kongano la viwanda Zuzu, kiwanda cha mafuta ya kula cha Pyxus Agriculture Tanzania limited, kiwanda cha mabati cha Dragon Limited na kiwanda cha Dane Holdings Limited.

Akizungumza katika kiwanda hicho, Prof. Mkumbo alisema ujenzi wa kiwanda hicho utakuwa mkombozi kwa kuwa na mbolea ya uhakika na kitazalisha mara nne ya kiwanda cha Burundi.

Alisema kiwanda hicho kinatarajiwa kukamilika Agosti, mwaka 2022 na kitasaidia upatikanaji wa bidhaa hiyo kwa bei nafuu.

"Ujenzi wa kiwanda hiki cha mbolea ni matunda ya ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyoifanya nchini Burundi, alikuta kiwanda cha mbolea ya asili cha Itracom Fertilizer Limited ambacho ni kikubwa kwa ukanda wa Afrika Mashariki na moja ya mazungumuzo ni kuwa kile kiwanda kijegwe pia hapa Tanzania na mara moja wawekezaji hawa walikubali kuja kujenga kiwanda hapa Dodoma," alisema.

Alisema ujenzi wake umefikia asilimia 35 na utagharimu Dola za Kimarekani milioni 180 na kuajiri wafanyakazi wa kudumu takriban 3,000 na kitakuwa na uwezo wa kuzalisha mbolea tani 500,000 kwa mwaka.

Aidha, alisema katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano unalenga kuzalisha ajira milioni nane na zinazozalishwa na kiwanda hicho ni utekelezaji wa mpango huo na kuwataka wakazi wa Dodoma kuchangamkia fursa hiyo.

Akiwa katika kiwanda cha mafuta ya kula cha Pyxus Agriculture Tanzania limited na mvinyo cha Dane Holdings Limited, Waziri Mkumbo alisema serikali imeendelea kuweka mkazo kwa wakulima kuzingatia kilimo bora na chenye tija ili kuwa na malighafi za kutosha kwa ajili ya viwanda.

Alitoa wito kwa benki zilizopo nchini kujikita kuwasaidia wajasiriamali wenye viwanda vidogo kwa kutoa mikopo yenye riba nafuu.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa Dodoma, Anthony Mtaka, alisema ujenzi wa kiwanda cha mbolea ukikamilika utainua uchumi wa Dodoma kutokana na wananchi kupata ajira nyingi na kusaidia kilimo cha zabibu kinachohitaji mbolea.

Naye msimamizi mkuu wa ujenzi wa kiwanda cha Itracom Fertilizer Limited, Rubenga Samson, alipongeza serikali kwa kuweka mazingira mazuri na vivutio vya kufanya uwekezaji nchini huku akiomba kuongezewa maji ambayo kwa sasa wanapata asilimia 10 ya mahitaji katika eneo la uwekezaji.





# Maduka 28 ya pembejeo yaanzishwa Nyanda za Juu

Na Grace Mwakalinga, MBEYA

MADUKA 28 ya pembejeo za kilimo yameanzishwa mikoa ya Nyanda ya Nyanda za Juu Kusini lengo likiwa kuwasaidia wakulima kupata mbegu na mbolea bora kwa wakati.

Ofisa Uhusiano wa Kampuni ya Ekari Moja Tanzania, Dorcas Tinga, alisema hayo wakati wa uzinduzi wa maduka 12 kati ya 28 ambayo yamezinduliwa mkoani hapa.

Alifafanua kuwa maduka 16 yalifunguliwa mkoani Njombe, tisa na matatu Songwe, yote yanakidhi vigezo vya utoaji huduma bora za pembejeo za kilimo.

"Katika kuhakikisha kampuni yetu inamjali mkulima tulianzisha programu ya kuwakopesha wakulima pembejeo za kilimo pamoja na mafunzo ili wazalishe kwa tija na kwamba hadi sasa wakulima 60,000 wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini wamenufaika," alisema Tinga.

Miongoni mwa wakulima wanaonufaika na kampuni hiyo, Teresia Mponzi kutoka Imezu, alisema elimu ya kilimo bora imekuwa msaada kwao kwa sababu wanalima kwa tija na kujiongezea kipato. Aliiomba Kampuni ya Ekari Moja kuendelea kutoa mikopo yenye riba nafuu na elimu ili wakulima wanufaike na kujikwamua kiuchumi.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, alisema serikali imetoa maelekezo kwa halmashauri zote kwa ajili ya kuimarisha sekta ya kilimo na kwa mwaka wa fedha 2021/2022 imetenga Sh. bilioni 187 kuimarisha kilimo nchini.

Aliipongeza Kampuni ya Ekari Moja kuwekeza katika utafiti na teknolojia ili kuongeza ufanisi wa huduma kwa wakulima kwa kuanza na vijiji vitatu vyenye wakulima 433 mwaka 2016.

Alisema hadi sasa jumla ya wakulima 6,957 wa vijiji 37 kwenye msimu wa kilimo 2021/2022 wamenufaika na wanaendelea kupata tija na manufaa kutoka kampuni hiyo.




Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Azania, Charles Itembe (aliyenyoosha mkono), akizungumza na baadhi ya wateja waliohudhuria hafla ya kifungua kinywa iliyoandaliwa na benki hiyo jijini Dar es Salaam juzi, kuadhimisha Wiki ya Huduma kwa Wateja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Miche milioni 1.6 ya matunda, mbao kuzalishwa

Na Grace Mwakalinga, RUNGWE

WILAYA ya Rungwe mkoani Mbeya kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wamepanga kuzalisha zaidi ya miche milioni 1.6 ya mbao, matunda na kivuli ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi na kuhifadhi mazingira wilayani humo.

Akizungumza na Nipashe juzi, Ofisa Maliasili wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Castor Makeula, wakati wa zoezi la uoteshaji wa miche ya kitalu kilichopo Kata ya Bulyaga mjini Tukuyu, alisema miche hiyo itagawiwa bure kwa wananchi kwenye sekta binafsi na umma kwa lengo la kuwawezesha wananchi kujikwamua kiuchumi kupitia biashara ya mbao na matunda.

"Tumeamua kuzalisha miche milioni 1.6 ya aina mbalimbali kama vile matunda, mbao na kivuli ikiwa ni hatua ya kuhifadhi vyanzo vya maji, kilimo na biashara ili kukuza uchumi wa wakazi wa Rungwe sambamba na utunzaji wa mazingira," alisema Makeula.

Vile vile, alisema kwa sasa wanaendelea kuzalisha miche hiyo na ifikapo Januari 2022 wananchi wataanza kugawiwa kwa kushirikiana na maofisa ugani kutoka kila kata za wilaya hiyo.

Baadhi ya wananchi walisema ni utaratibu mzuri ulioanzishwa na wilaya kuwagawia miche ili kuendeleza jitihada za kuhifadhi mazingira na kwamba wataendelea kuitunza kwa manufaa ya kizazi cha sasa na baadaye.

Miongoni mwa wananchi hao, Mary Mwangupili wa Kijiji cha Ilolo alisema ni mara kadhaa amekuwa akipewa miche ya matunda na mbao na viongozi wa wilaya hiyo na ameanza kunufaika kwa kuuza parachichi na kujiingiza kipato.

Aliishukuru serikali na kuishauri kuongeza jitihada kutunza chanzo cha maji cha Mto Kilasi ili kiendelee kutoa maji katika kipindi chote cha mwaka na kupanda miti.

# Waomba barabara wapate huduma muhimu

Na Grace Mwakalinga, RUNGWE

WANANCHI wa vijiji vya Kyobo Juu na Kyobo Chini vilivyopo Kata ya Ikuti, wilayani Rungwe wameiomba serikali kuwasaidia kujenga barabara yao waliyoilima kwa mkono miaka mingi iliyopota ili magari yaweze kupita.

Wakizungumza kwenye mkutano wa hadhara ulioandaliwa na Mkuu wa Wilaya Rungwe, Dk. Vicent Anney, wananchi hao walisema kuwa barabara pekee inayoingia kwenye vijiji hivyo walilima wenyewe kwa mikono miaka mingi iliyopita na haijawahi kukwatuliwa na greda.

Deus Mwaijumba alisema kuwa kwa namna barabara hiyo ilivyolimwa na wazee wao miaka mingi iliyopita, magari hayawezi kupita na kuvifikia vijiji vyao na kuomba msaada wa serikali iiboreshe ili iweze kupitika.

"Barabara hii ambayo ndiyo inaingia kwenye vijiji vyetu vya Kyobo Juu na Kyobo Juu haijawahi kutumiwa na magari tangu nchi ipate Uhuru, hii ni kwa sababu ililimwa kienyeji na wazee wetu kwa kutumia jembe la mkono miaka mingi iliyopita, tunaomba sasa serikali itusaidie kuilima kwa greda ili magari yapite na kufika kwenye vijiji vyetu," alisema Mwaijumba.

Alisema katika vijiji hivyo wanazalisha mazao mengi ya biashara na chakula kama ndizi, iliki, kahawa, magimbi na mihogo, lakini hawawezi kuyasafirisha kwa wingi kwenda kuyauza.

"Tunayo mazao yetu tunayolima kwa wingi, ingawa tunajua yana soko kubwa nje ya vijiji vyetu, lakini tunashindwa kuyasafirisha kwa wingi na hata wanunuzi wanashindwa kuja kuyanunua kwa sababu hakuna barabara, baadhi yetu tunalazimika kuyabeba kichwani kwenda kuyauza ili tupate fedha za kujikimu, tunaomba tusaidiwe barabara kuondokana na kero hizi," alisema Mwaijumba.

Kwa upande wake Lucia James, alisema kuwa ukosefu wa barabara pia una athari kubwa kwa wanawake hasa wajawazito wanapohitaji kujifungua wanapotaka kwenda kwenye vituo vya afya.

Alisema usafiri pekee unaowasaidia wajawazito kwenda kujifungua kwenye vituo vya afya ni pikipiki, usafiri aliodai kuwa sio rafiki kwao hasa wenye matatizo ya uzazi.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Mpokigwa Mwankuga, akaungana na wananchi hao kuomba msaada wa ujenzi wa barabara hiyo, akisema kuwa Serikali Kuu inapaswa kutenga bajeti ya kuwasaidia wananchi hao katika mwaka ujao wa fedha.

Mwakilishi wa Meneja wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) Wilaya ya Rungwe, Mhandisi Senyange Kayoka, alisema jukumu la wakala huo ni kufungua barabara kwenye maeneo yote ili wananchi wazitumie kwa shughuli za maendeleo.

Aliahidi kuwa katika mwaka ujao wa fedha barabara hiyo itakuwa ya kwanza kuingizwa kwenye bajeti ya TARURA ili iweze kujengwa na kumaliza kero ya wananchi hao.

Akizungumza na wananchi hao, Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Anney, alisema atasimamia kikamilifu kuhakikisha barabara hiyo inapitika kwa gari kwa manufaa na maendeleo ya wananchi wa vijiji hivyo.

Alisema barabara hiyo ikifunguka anaamini wananchi hao watapata maendeleo ya haraka kwa vile ni wazalishaji wazuri wa mazao ambayo yanapendwa na yenye soko la uhakika ndani na nje ya Wilaya ya Rungwe.





## Othman aagiza mpango uchimbaji, upatikanaji mawe

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, ameviagiza vyombo vinavyosimamia rasilimali za ardhi kukaa pamoja kuandaa mpango utakaoweka utaratibu bora wa upatikanaji na uchimbaji wa mawe nchini bila kuwepo uharibifu mkubwa wa mazingira.

Othman, aliyasema hayo juzi Fumba Wilaya ya Magharib 'B' Unguja katika ziara maalum ya kutembelea maeneo mbalimbali yenye uharibifu wa mazingira unaotokana na mabadiliko ya tabianchi pamoja na shughuli zinazofanywa na binadamu.

Alisema yapo maeneo mengi ambayo yameathirika kutokana na kuchimbwa mawe bila kuwapo utaratibu, hivyo kusababisha athari kubwa za kimazingira, lakini ni vyema katika mpango utakaoandaliwa kutengwa maeneo maalum ya uchimbaji wa mawe kwa utaratibu wa kutapunguza kasi ya athari za mazingira.

Alisema kwa vile rasilimali hiyo ni muhimu, itaendelea kuhitajika na wananchi kwa shughuli mbalimbali za kijamii, lakini mamlaka zinazohusika hazinabudi kuandaa utaratibu sahihi ikiwamo mpangilio bora na kufanya juhudi za urejeshaji wa eneo lililotumika kwa kuchimbwa mawe katika hali ya asili ili kutumika kwa shughuli zingine ikiwamo za kilimo na kuwa mbadala wa kuwasaidia wananchi.

Aidha, aliutaka uongozi wa Kampuni ya ZANARAB Metel ya Zanzibar inayojishughulisha na kazi za ukusanyaji, ufungaji na usafirishaji wa vyuma chakavu kuwa makini na kuepuka kushirikiana na wahalifu wanaoharibu miundombinu ya maendeleo ya nchi.

Alisema kuwapo kwa kampuni hiyo ni juhudi muhimu katika kuwasaidia vijana kupata ajira, lakini ameutaka uongozi wa kampuni hiyo kutokaribisha uharibifu wa miondombinu ya kimaendeleo na badala yake waweze kusaidia serikali katika kuilinda miundombinu ya maendeleo ya kimaendeleo isihujumiwe na wahalifu.

Wakati huo huo, Makamu wa Kwanza wa Rais ameupongeza wanaushirika wa ustawi wa jamii wanaojighulisha na upandaji wa mikoko na uhifadhi wa mazingira huko Chuwini Wilaya ya Magharibi 'A' Unguja kwa juhudi zao na kuendeleza uhuifadhi wa mazingira na kwamba serikali inaunga mkono juhudi hizo.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Dk. Saada Mkuya Salum, alishauri uongozi wa Kampuni inayojishughulisha na utunzaji wa mazingira kujiandaa kuzifikia taasisi za fedha kwa ajili ya kupata mikopo ya kuendeleza biashara zao.

Alisema iwapo kampuni zinaandaa mpango bora wa kibiashara, lakini wanayofursa kubwa ya upatikanaji wa mikopo kutoka benki mbalimbali ili kuendeleza biashara zao.

Mmliki wa Kampuni ya ZANARA, Ali Issa, alisema kwamba kampuni yake imekabiliwa na changamoto mbalimbali vikiwamo vibali vingi vya biashara na kuiomba serikali kuangalia suala hilo ili kurahisisha uendeshaji wa shughuli zao za biashara na kusaidia upatikanaji wa ajira kwa vijana.

Akitoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanziba, Sheha Mjaja, alisema kwamba utafiti mbalimbali zilizofanywa zimebaini kuwapo maeneo yaliyoharibika kimazingira na kwamba serikali imeandaa mpango wa muda mfupi na muda mrefu katika kukabiliana na athari za kimazingira Zanzibar.

# Wenye kichwa kikubwa, mgongo wazi waongezeka

**Na Rahma Suleiman**, ZANZIBAR

DAKTARI wa Kitengo cha Upasuaji wa Kichwa na Uti wa Mgongo, Omar Muhamed Mussa, amesema idadi ya watoto wenye tatizo la kichwa kikubwa na mgongo wazi inaongezeka Zanzibar.

Amesema tatizo hilo limeongezeka kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ukosefu wa lishe kwa mama mjamzito.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari katika Hospitali ya Mnazi Mmoja Mjini Unguja, kuhusu maadhimisho ya Siku ya Vichwa Maji na Migongo Wazi ambayo kitaifa huadhimishwa Oktoba 23, kila mwaka.

Alisema kuwa kitengo hicho kimepokea wagonjwa wa vichwa maji 224 kutoka mwaka 2017 hadi 2021 ambapo 165 wakaazi wa Unguja, 45 Pemba na 14 Tanzania Bara na waliofariki ni wanane.

Alisema kwa upande wa wagonjwa wa mgongo wazi kwa miaka hiyo wamepokea wagonjwa 61 ambao kati ya hao wanawake ni 32 na wanaume ni 29 na waliofariki kutoka 2017 mpaka 2021 ni 14.

"Tatizo la mgongo wazi na vichwa maji mara nyingi vinakwenda sambamba, hivyo niwaombe waandishi wa habari kutoa elimu kwa jamii kuhakikisha kinamama wanapokuwa wajawazito kula vyakula vyenye vitamini vya Folic acid ambapo miongoni mwa vyakula hivyo ni matunda, mboga na vyakula vya nafaka," alisema.

"Gharama za huduma za watoto hao ni kubwa na mama ni mwathirika mkuu wa kuhudumia mtoto licha ya kwamba wanaume tunasaidia kutoa huduma, lakini mama ndio anayehangaika na mtoto," alisema.

Daktari huyo alisema kuwa matibabu ya wagonjwa hao yanatolewa bure hospitalini hapo, hivyo aliwataka wazazi wenye watoto wenye tatizo hilo kuwapeleka hospitali ili kupata matibabu yanayostahiki.

Naye Katibu wa Jumuiya ya vichwa maji na mgongo wazi, Hussein Muhammed Saleh, alisema kuwa jumuiya hiyo imetafuta nyumba kwa ajili ya kuwasadia watoto hao kuishi wakati wanapoendelea na matibabu.

Alieleza kuwa wengi wa watoto wenye vichwa maji na migongo wazi huwa wanapata usumbufu mkubwa wa kupata makazi hasa wale wanaotoka nje ya Unguja wanapopata huduma ya matibabu ikiwamo upasuaji katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

"Wazazi wenye watoto wa vichwa maji na vichwa vikubwa ambao wanatoka vijijini au nje ya kisiwa cha Unguja huwa wanafikia kwa jamaa zao, lakini baadhi yao huwa wananyanyapaliwa kutokana na hali walizonazo, hivyo tumeamua kuwatafutia nyumba kwa muda wote wanapokuwa wanapata matibabu ambapo nyumba hiyo hupatiwa huduma zote muhimu bila ya malipo," alisema.

Rahma Mkanga, mama mwenye mtoto wa kichwa maji na mgongo wazi alisema bado baadhi ya familia zinaimani za kishirikina kuhusu kuzaa mtoto mwenye tatizo hilo.

Alisema baadhi ya wanaume huwatelekeza watoto wao wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi na hatimaye mzigo wote humwelemea mama wa mtoto bila ya kupata msaada wowote kutoka kwa baba wa mtoto.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, Masoud Ali Mohammed (kushoto), akizungumza na wajumbe wa Tume ya Haki za Binadamu, walipofika ofisini kwake mjini Zanzibar jana, kwa ajili ya kujitambulisha. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Tume yatoa mafunzo ya haki za binadamu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TUME ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Tanzania, imeanza kutoa mafunzo kwa makundi mbalimbali ya jamii kuhusu haki za binadamu na utawala bora ili kulinda na kutetea haki hizo.

Hayo yalisema juzi na Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji mstaafu Mathew Mwaimu, wakati akizungumza na waandishi wa habari Mjini Zanzibar.

Alisema mafunzo hayo yatawafikia wananchi 400 kwa mikoa mitatu ya Zanzibar ili kukabiliana na changamoto mbalimbali ikiwamo ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto ambayo yanalikabili Taifa.

"Tupo hapa Visiwani Zanzibar kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa wananchi na mafunzo hayo tunaanza kutoa ambayo ya siku tano," alisema mwenyekiti huyo.

Alieleza kuwa wananchi watakaofaidika na mafunzo hayo ni viongozi wa Serikali za Mitaa, viongozi wa madhehebu ya dini, wanawake na wanafunzi wa ngazi mbalimbali.

Alisema kuwa mafunzo hayo ni sehemu ya utekelezaji wa mpango mkakati wa Tume wa miaka mitano ambapo moja ya malengo yake ni kukuza haki za binadamu na utawala bora nchini.

"Tume inatoa mafunzo hayo visiwani Zanzibar kama sehemu ya mchango wake katika jitihada za wadau za kukabiliana na kadhia ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto inayoelekea kushamiri Zanzibar," alisema.

Aidha, alisema licha ya jitihada za serikali na wadau za kukabiliana na tatizo la ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto bado vitendo hivyo vinaendelea kuongezeka ambapo kwa mujibu wa takwimu kutoka kwa mtakwimu mkuu wa serikali, matukio 116 yameripotiwa katika vituo vya Polisi kwa Januari mwaka 2020 na matukio 122 kwa Januari mwaka huu.

Mwenyekiti huyo alieleza kuwa hali hiyo inaashiria kuwa watoto hawako salama na jamii isipochukua hatua za makusudi na za haraka, maisha ya watoto yatakuwa hatarini.

## HABARI KITAIFA




Mratibu wa Mradi wa Taasisi isiyo ya Serikali ya Feet Tanzania, Alfred Kiuyo (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa programu ya Stem, kwa ajili ya kuwajengea uwezo watoto wa kike kupenda kusoma masomo ya Sayansi, kama sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kike Duniani. Kulia ni Mratibu Msaidizi wa taasisi hiyo, Salmin Kigondo na mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Temeke, Naellah Martin. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Serikali yapata dawa ya uhaba wa mbolea

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Kilimo, Prof. Aldof Mkenda, amesema serikali imepanga kufufua kampuni ya mbolea iliyokuwa ikiitwa Tanzania Fertilizer Company ili isaidie kuanzisha viwanda vingi vya bidhaa hiyo nchini na kupunguza tatizo la uhaba wa bidhaa hiyo uliopo.

Prof. Mkenda alitoa kauli hiyo jana mjini Songea mkoani Ruvuma katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mbolea Duniani ambayo kitaifa ilifanyika mkoani humo.

"Serikali iko kwenye mpango wa kufufua kampuni ya mbolea ili washiriki kusambaza mbolea nchini, na tunaamini kwamba kufufuliwa kwa kampuni hii, kutasaidia kuanzisha viwanda vingine vya mbolea nchini na hivyo kutatua tatizo la upungufu wa bidhaa hiyo uliopo kwa sasa.

"Kama tunanunua mbolea ambayo inazalishwa na kampuni nyingine ya nje, tunashindajwe kufufua kampuni yetu ili huko mbeleni tuhakikishe kwamba hatupati changamoto za upungufu wa mbolea kirahisi," alisema.

Pia alisema serikali itaimarisha huduma na taarifa za afya ya udongo maeneo yote ili kuhakikisha wakulima wote wanafahamu aina ya mbolea wanayopaswa kuitumia kwenye mazao zao.

Prof. Mkenda alisema tayari serikali imeongeza fedha kwa ajili ya maofisa ugani na kwamba kwa sasa wataanza na mikoa mitatu kuwapa pikipiki, vitendea kazi na mafunzo rejea ikiwa ni pamoja na mafunzo ya namna ya kupima udongo ili kushauri wakulima aina ya udongo wanaotakiwa kuutumia.

"Tunajipanga kuhakikisha mkulima anatumia mbolea ambayo inamwongezea tija kwenye kilimo chake, tutaendelea kuhimiza wabunifu mbalimbali ili waongeze uzalishaji wa mbolea hiyo, ili tuweze kuzalisha mbolea nyingi nchini na kuzitumia," alisema Prof. Mkenda.

# Bil. 19/- kujenga Ofisi ya Makamu wa Rais

**Na Mwandishi Wetu**

OFISI ya Makamu wa Rais imetia saini mkataba wa Sh. bilioni 18.8 na Kampuni ya Ujenzi ya SUMA JKT wa kuanza awamu ya pili ya ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais katika Mji wa Serikali Mtumba jijini Dodoma.

Hafla ya kutia saini mkataba wa ujenzi huo ilifanyika jana katika Ofisi ya Makamu wa Rais Mtumba jijini Dodoma na kukabidhi rasmi eneo la ujenzi kwa mkandarasi baada ya kushinda zabuni na kushuhudiwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) ambaye ndio Msimamizi Elekezi wa ujenzi wa jengo hilo.

Akizungumza katika hafla hiyo, Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Mary Maganga, alipongeza SUMA JKT kwa kushinda kandarasi hiyo na kutaka ujenzi uwe wa haraka kwa kuzingatia ubora, viwango na kasi.

"Ninaamini kuwa SUMA JKT mna uzoefu mkubwa na ujenzi huu utaenda kwa kasi na kuzingatia viwango vya ubora wa hali ya juu, na ikiwezekana mkamilishe kazi hii kabla ya muda uliopangwa," alisema.

Katibu Mkuu alisema kukamilika kwa jengo hilo kutaongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu kwa kuwa serikali ilipohamia Dodoma, jengo lililojengwa katika eneo la Mtumba halitoshelezi mahitaji ya watumishi wote, hivyo kulazimika kutumia jengo lingine mjini kwa ajili ya watumishi wa idara zingine.

"Wenzetu wa Idara ya Mazingira wapo wengi na wana majukumu mengi, kila tunapowahitaji kuja kwa ajili ya vikao, inabidi waje huku Mtumba. Kwa hiyo jengo hili likikamilika ndani ya muda, tuna imani ufanisi utaongezeka na tunaweza kufanya kazi kwa pamoja na muda tunaotumia barabarani utapungua au kuondoka kabisa," alisema.

Mary alisema msimamizi wa ujenzi huo, NHC, atafanya kazi kwa karibu na Kamati ya Ujenzi ya Ofisi ya Makamu wa Rais inayoongozwa na Naibu Katibu Mkuu, Mohammed Khamis Abdullah, na kusisitiza kutenga ofisi kwa ajili ya Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

"Ofisi ya Makamu wa Rais ndio wasimamizi wa masuala ya Muungano na mazingira nchini, hivyo tutatoa nafasi katika jengo hili jipya kwa ajili ya wenzetu wa Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za Serikali kwa upande wa Zanzibar kupata nafasi ili kurahisisha masuala ya uratibu wa utekelezaji wa majukumu ya serikali kwa pande zote mbili za Muungano," aliongeza.

Mhandisi Morgan Nyonyi kutoka SUMA JKT, alimwahidi Katibu Mkuu kuwa SUMA JKT watatekeleza mradi huo kwa ustadi mkubwa kwa kuhakikisha wanakamilisha mradi huo wa ujenzi kwa wakati na ikiwezekana kabla ya miezi 24 iliyopo ndani ya mkataba.

"Tutajitahidi kwenda na wakati na kuzingatia viwango vya ubora, rasilimali fedha na rasilimali watu tunao wa kutosha. Naishukuru serikali kwa kutoa kiasi kikubwa cha fedha zitakazowezesha kutekelezwa kwa mradi huu na Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kutuamini SUMA JKT," alisema.

Meneja wa Huduma za Kihandisi wa NHC, Manning Mwalaka, alisema shirika litahakikisha mkandarasi anafuata taratibu zote za ujenzi kwa mujibu wa mkataba katika kipindi chote cha utekelezaji wa mradi.

"Sisi na NHC tumepewa dhamana ya kuwa wasimamizi katika mradi huu, tutashirikiana kwa pamoja na kuhakikisha kwamba hili jengo linajengwa kwa viwango vilivyokusudiwa," alisema. Kukamilika kwa ujenzi wa jengo hilo kunatarajiwa kutimiza lengo la Ofisi ya Makamu wa Rais kuhakikisha idara na vitengo vyake vyote vinahamia kwenye jengo hilo na kufanya kazi kwa pamoja.

# DAWASA yalipa fidia kwa waliopisha mradi

**Na Frank Monyo**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), imelipa jumla ya Sh. milioni 236.6 kwa ajili ya fidia kwa wakazi saba wanaopisha ujenzi wa mradi wa maji Mshikamano, Jimbo la Kibamba.

Mradi huo wenye thamani ya Sh. bilioni 5.4 unaotekelezwa kati ya DAWASA na Kampuni ya Advent Construction Limited kwa miezi miezi 12 kuanzia Oktoba 15 kesho na tayari umekwishatiwa saini chini ya Waziri wa Maji, Jumaa Aweso.

Akishuhudia makabidhiano ya mfano wa hundi kwa wakazi hao juzi, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, aliwashukuru wananchi hao waliotoa maeneo yao ili mradi huo utekelezwe na kuwaomba wananchi wengine kutoa ushirikiano kwa DAWASA ili kuhakikisha mradi huo.

Makabidhiano hayo yalifanya kwenye Bohari Kuu ya DAWASA, Boko, Dar es Salaam ambapo Makalla alianza kwa kukagua vifaa mbalimbali ikiwamo mabomba makubwa na madogo yatakayotumika kwenye mradi huo na maeneo mengine ikiwamo Mwabepande, Chanika na pembezoni.

"Leo ni mara ya pili ninakuja hapa, nilikuja hapa nikiwa naibu waziri wa maji na hapa ndipo panaitwa bohari na hapakuwa hivi. Ilikuwa ni bohari isiyokuwa na kitu ila leo ni bohari iliyosheheni vifaa mbalimbali. Nikupongeze sana CEO (Cyprian Luhemeja) kwa haya, kwani yanatoa matumaini kuwa mmejipanga kutoa huduma na uwezo mnao," alisifu.

Makalla aliongeza: "Nimefurahi namna ambavyo DAWASA mmekuwa wepesi sana wa kushughulikia kero na kuwa karibu na ofisi ya mkuu wa mkoa.

"Mimi nimewapima taasisi katika ziara ya kutatua kero za wananchi jimbo kwa jimbo, hakuna sehemu DAWASA mmekosa, mnaonyesha mko tayari kuwahudumia wananchi."

Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Cyprian Luhemeja, alisema miongoni mwa maelekezo waliyopewa ni kuhakikisha wanapeleka huduma ya maji maeneo ya pembezoni na tayari wameanza kufanyia kazi ikiwamo Jimbo la Kibamba.

"Kwa sasa tunahakikisha tunakuwa na mabomba ya kutosha ya ukubwa mbalimbali na vifaa ili kumaliza kabisa tatizo la upatikanaji wa maji," alisema.

Luhemeja alimweleza Makalla kwamba mchakato wa kuwa na gharama moja kwa wateja wote wa majumbani ya kuwaunganishia umefanyiwa kazi na wamewasilisha kwa bodi ili wakiidhinisha, utaitangazwe kwa wananchi.

Maeneo yatakayonufaika na mradi huo utakapokamilika ni Mpiji, Mshikamano, Magohe, Msakuzi Kaskazini, Machimbo, Majengo Mapya, Dodoma, Luguruni Lapaz, Mbezi Inn, Magari saba, Magayana na Njia Panda Makondeni.

Mengine ni Kwa Gamba, Takukuru, Luguruni Dampo, Luguruni KKKT, Rising Star, Msakuzi Supermarket, Aman Street, Miti Mirefu, Madafu, Kwa mfala, Chikongwe, Masaki Street, Mbezi Msumi, Machimbo na Mageti.

# AZAM YAPANGA KUWAKABILI PYRAMIDS MAPEMA MCHANA

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Azam FC imesema mechi yao ya raundi ya kwanza ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Pyramids kutoka Misri itachezwa kuanzia saa 9:00 mchana keshokutwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, jijini Dar es Salaam.

Ofisa Habari wa Azam FC, Thabit Zacharia, alisema mpaka sasa bado hawajapata taarifa yoyote kutoka Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kama watapata ruhusa ya kuingiza mashabiki, lakini juhudi bado zinafanywa ili kuomba ruhusa.

Zakaria alisema uamuzi wa kucheza mchana umefanywa kwa mapendekezo kutoka kwa benchi la ufundi na si kulenga kuwachosha wapinzani wao.

> **"Sijafanya utafiti wa kutosha kuwa Waarabu wanapata tabu wakicheza kwenye mazingira ya jua kali, lakini mimi ninavyojua tupo ndani ya kanuni wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF) inayosema unaruhusiwa kucheza mechi za kimataifa muda wowote kuanzia saa 9:00 alasiri hadi saa nne usiku, kwa hiyo sisi tumeamua kucheza muda huo," alisema Zacharia.**

Aliongeza timu yao inaendelea vyema na maandalizi na wanaamini wachezaji watapambana kuhakikisha wanapata matokeo mazuri na kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kusonga mbele.

"Tena kama maombi yetu yatakubaliwa ya kuingiza kiasi cha mashabiki kama tulivyoomba CAF kupitia TFF (Shirikisho la Soka Tanzania), itakuwa vizuri zaidi kwa sababu mechi ikianza muda huo itaisha mapema na mashabiki watarudi makwao mapema sana," Zacharia alisema.

Alisema pia kikosi chao kimeendelea kuimarika na mchezaji ambaye ni majeruhi ni Prince Dube, huku akiwatoa hufu mashabiki wa Azam waliokuwa na wasiwasi juu ya wachezaji wao waliokwenda kuzitumikia klabu zao za taifa kwenye michuano ya kusaka tiketi ya kucheza Kombe la Dunia mwakani nchini Qatar Ukanda wa Afrika, kuwa wote wamesharejea.

"Tunashukuru kikosi kimekamilika, wachezaji waliokwenda kutumikia mataifa yao wote wamesharejea na wanaendelea na programu za klabu, akili yetu ni kuona tunapambana ili kupata matokeo mazuri hapa nyumbani na baadaye kwenda Misri kukamilisha kazi," aliongeza kiongozi huyo.

Pyramids ilitarajiwa kuwasili nchini jana saa 3:00 usiku tayari kwa mechi hiyo, huku mchezo wao wa marudiano ukitarajia kuchezwa Oktoba 23, mwaka huu nchini Misri.

Timu nyingine za Tanzania zilizobakia katika mashindano ya kimataifa ni Biashara United ya Musoma inayopambana kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika wakati mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba wao wanapeperusha bendera ya nchi katika kinyang'anyiro cha Ligi ya Mabingwa Afrika.

# *Gwomeka ashinda Jackpot bonus*

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Ngara, Bukoba Expectance Gwomeka ameibuka mshindi wa bonus ya Jackpot ya wiki iliyopita kutoka SportPesa ambapo aliweka bet mbalimbali za jackpot na kufanikisha kwenye bet moja.

Akizungumza wakati wa mahojiano katika ofisi za Sportpesa, Expectance alisema "Mimi ni mfanyabiashara na vile vile ninajishughulisha na kilimo kama sehemu inayoniingizia kipato.

"Ni muda kidogo tangu nianze kubashiri kwani nilikuwa nikihamasishwa na baadhi ya washindi waliopita wa bonus lakini hasa ni washindi wa Jackpot ambao wameweza kushinda milioni kuanzia Sh. milioni 300 hadi 400. Nikaona na mimi nianze kucheza huenda siku nitashinda."

"Pesa niliyoipata itaenda kuendeleza kilimo na kuboost biashara moja kwa moja kwani kule kwetu sasa hivi ni msimu wa kupanda mahindi, maharage kwa hivyo hii pesa imekuja muda muafaka."

"Nawasihi wapenda michezo wazidi kujiongeza na kuanza kubashiri na SportPesa kwani baada ya mechi kuisha kama utaibuka mshindi utawekewa pesa zako kwenye akaunti ya Sportpesa moja kwa moja".




Mshindi wa bonus ya Jackpot, Expectance Gwomeka kutoka Ngara, Kagera akishikilia mfano wa hundi ya Sh. milioni 21.1 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya wiki iliyopita. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Polisi Tanzania yaimarisha ulinzi

**Na Saada Akida**

ILI kujiweka katika nafasi salama kuelekea mchezo wao dhidi ya Mabingwa watetezi wa Ligi Kuu, Simba, Kocha Mkuu wa Polisi Tanzania, Malale Hamsini amesema analazimika kuboresha zaidi mbinu za wachezaji wake hasa kwenye eneo la ulinzi.

Polisi Tanzania itasafiri kwenda Dar es Salaama kuwafuata Simba katika mchezo wa Ligi Kuu Bara utakaochezwa Oktoba 27, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Malale alisema amekiangalia vizuri kikosi cha Simba na kubaini kina safu ya washambuliaji wenye 'kiu' licha ya kuanza msimu mpya kwa kupata sare na kushinda mechi ya pili ugenini.

Kocha huyo alisema kamwe hatawadharau wapinzani wake na ataendelea na maandalizi kuelekea mchezo kwa sababu anawaheshimu na kuitambua Simba ina safu imara ya ushambuliaji.

"Tunahitaji kuendelea kufanya vizuri katika michezo yetu yote ili kujiimarisha na kubakia kileleni, tunatakiwa kujipanga vizuri hasa kwa mechi yetu ijayo ambayo itakuwa ya ushindani mkubwa kwa sababu Simba ina wachezaji wazuri."

## Tamasha la Makete kufanyika Novemba Dar

**Na Beatrice Shayo**

TAMASHA la kuonyesha mila na desturi za Wanamakete ambalo litajumuisha burudani za ngoma za asili na maonyesho ya mavazi ya asili limepangwa kufanyika Novemba mwaka huu kwenye Kijiji cha Makumbusho jijini Dar es Salaam, imefahamika.

Katibu wa Chama cha Maendeleo ya Wanamakete (MDA), Award Mpandilah alisema tamasha hilo litakuwa na siku tatu na lengo lake ni kuwaunganisha wanajamii wote wanaoishi ndani na nje ya Wilaya ya Makete.

Mpandilah alisema tamasha hilo la utamaduni wa Mtanzania ni utaratibu uliowekwa na Bodi ya Makumbusho ya Taifa tangu mwaka 1994 ili kuzipa jamii za Kitanzania kuonyesha mila na desturi zao katika Kijiji cha Makumbusho kila mwaka.

"Tutakuwa na semina na warsha zitakazoongelea kwa mapana historia mila na desturi pamoja na maendeleo ya Makete, kiafya, miundombinu, kilimo, utalii pamoja na hali ya uchumi kwa ujumla," Mpandilah alisema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### HAALAND, CITY KUTETA

WAKALA wa Erling Braut Haaland, Mino Raiola, 21, anatarajiwa kufanya mazungumzo na Manchester City kuhusu uwezekano wa uhamisho wa mshambuliaji huyo wa Borussia Dortmund na Norway ifikapo msimu ujao wa majira ya joto. ***(Times)***

### STERLING AIBANA CITY

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya England, Raheem Sterling, 26 anataka kuhakikishiwa kwamba ni sehemu muhimu ya mipango ya Pep Guardiola kabla ya kuanza tena mazungumzo ya mkataba na Manchester City. ***(Sun)***

### CHAMBERLAIN SOKONI

LIVERPOOL iko tayari kumuuza kiungo wa kati wa England, Alex Oxlade-Chamberlain, 28, lakini kwa bei stahiki huku klabu yake ya zamani ya Arsenal ikimtaka. ***(Mirror)***

### DEMBELE ANUKIA LIVERPOOL

LIVERPOOL pia imeanza majadiliano ya kumsajili mshambuliaji wa Barcelona Mfaransa, Ousmane Dembele, 24, kwa uhamisho wa bure msimu huu wa joto. ***(Mail, via Mundo Deportivo)***

### FODEN MAMBO MAZURI

KIUNGO wa kati wa England, Phil Foden, 21, anakaribia kusaini mkataba mpya na Manchester City. Mkataba wake wa sasa unamalizika ifikapo mwaka 2024. ***(The Athletic)***

### TCHOUAMENI AGOMBEWA

MANCHESTER United wameungana na Chelsea na Juventus katika mbio za kumsaka kiungo wakati wa Monaco na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Aurelien Tchouameni mwenye umri wa miaka 21. ***(Express)***

### LENGLET KIMEELEWEKA

MLINZI wa Barcelona, Clement Lenglet , 26, huenda akawa wa kwanza kuwasili Newcastle United baada ya klabu hiyo kununuliwa hivi karibuni. ***(Sport.es)***

### BELLERIN AIKATAA ARSENAL

MCHEZAJI wa Hispania, Hector Bellerin, 26, amedokeza hana nia ya kurejea Arsenal pale mkataba wake wa mkopo wa msimu mzima utakapomalizika Real Betis. ***(El Desmarque, via Mail)***

### RUDIGER NJIA PANDA

MLINZI wa Ujerumani, Antonio Rudiger, 28, anatathmini hali ilivyo kabla ya kufanya uamuzi juu ya mustakabali wake katika klabu ya Chelsea, huku mkataba wake wa sasa ukitarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Sky Sports)***

### JOHNSTONE AGEUKA LULU

KLABU za Southampton, Tottenham na West Ham zinataka kumsajili golikipa wa West Brom na England, Sam Johnstone, 28. ***(Hampshire Live)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# RONALDO AFUNGUKA ATAKA MAKUBWA

**Mshambuliaji huyo asisitiza ni 'hulka' yake kuhitaji mafanikio zaidi na...**

**LISBON,** Ureno

CRISTIANO Ronaldo amesema aliahidi "mara zote nataka zaidi na zaidi" baada ya kufunga 'hat-trick' wakati Ureno ikiifumua Luxembourg kwenye mchezo wa kufuzu michuano ya Kombe la Dunia mwakani.

Ronaldo alifunga 'hat-trick' yake ya 58 kwenye maisha yake ya soka na ya 10 kwa Ureno wakati Selecao wakipata ushindi rahisi wa mabao 5-0 dhidi ya Luxembourg hapo juzi Jumanne.

Mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or mwenye umri wa miaka 36, alifunga penalti mbili ndani ya dakika tano mapema kipindi cha kwanza na alifunga bao lake la tatu zikiwa zimebakia dakika tatu mchezo kumalizika.

**Mabao mengine ya Ureno katika mchezo huo yalifungwa na Bruno Fernandes na Joao Palhinha.**

Ureno imepitwa pointi moja kwenye Kundi A na vinara Serbia, ingawa wana mchezo mmoja mkononi, katika mbio hizo za kuwania kwenda nchini Qatar.

Ronaldo ambaye aliongeza mabao aliyofungua akiwa na Ureno na kufikia 115 aliandika kupitia Instagram: "Ushindi mwingine, hatua nyingine, usiku mwingine wa historia kutetea rangi ya jezi zetu!

"Kila kitu kinakuwa rahisi wakati tunapocheza nyumbani mbele ya mashabiki wetu na tunapambana.

"Nilishawahi kuahidi mara zote nitakuwa nataka zaidi na zaidi!

"Hiyo ndiyo hulka yangu na hulka yetu, mara zote hatusalimu amri kwani tunapambana kusonga mbele."

MECHI KALI
HOME
AWAY
BOLIVIA
2.31 | 3.14 | 3.24
PARAGUAY

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 576

# KANE ATAJWA NEWCASTLE



**LONDON,** England

NAHODHA wa zamani wa Newcastle United, Rob Lee amesema "nitapenda" kama Harry Kane atatua klabuni hapo baada ya Kevin Keegan kuonyesha hisia za jambo hilo kutokea.

Kane na timu yake ya Tottenham Hotspur watasafiri kwenda kwenye Uwanja wa St. James' Park Jumapili kucheza mchezo wa kwanza na Newcastle tangu inunuliwe.

Klabu hiyo sasa inamilikiwa na Kampuni ya uwezekaji wa Umma ya nchini Saudi Arabia (PIF) chini ya mwana wa mfalme, Bin Salman pamoja na Amanda Staveley, ambaye ana hisa asilimia 10.

PIF, imenunua asilimia 80 ya Newcastle na kuifanya kuwa klabu tajiri zaidi duniani, na hivyo kuwa na ushawishi wa kusajili wachezaji wenye majina makubwa.

Kane hajawa jina linalotajwa sana, lakini alitaka kuihama klabu yake ya Spurs kabla ya kuanza kwa msimu huu na sasa Keegan, kocha wa zamani wa Newcastle alionyesha hisia Kane anafaa kutua hapo, huku akiungwa mkono na Lee.

Nahodha huyo wa England amefunga mabao matano ya Ligi Kuu nchini humo akicheza kwenye Uwanja St James' Park.

# Denmark yapata tiketi Kombe la Dunia

**COPENHAGEN,** Denkar



DENMARK imekuwa timu ya pili kufuzu kucheza michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2022 nchini Qatar baada ya kuifunga Austria 1-0 katika mchezo wa Kundi F.

Shuti la kipindi cha pili la Joakim Maehle lilimshinda Franco Foda na kujaa wavuni katika mechi iliyochezwa juzi Jumanne na kuifanya Denmark kuongoza kundi hilo kwa pointi saba dhidi ya Scotland huku zikiwa mebaki mechi mbili za kucheza.

Ushindi huo unamaanisha kikosi hicho cha kocha, Kasper Hjulmand kimeweka rekodi nzuri zaidi ya kufuzu kwa Kombe la Dunia, baada ya kushinda mechi zote nane bila kuruhusu bao.

Denmark imefunga mabao 27 dhidi ya Moldova, Israel na Austria na sasa imefuzu kwenda Kombe la Dunia ikitoka kutinga nusu fainali ya Euro 2020 kabla ya kuondolewa na England kwenye muda wa ziada.

Sasa limekuwa taifa la pili kufuzu baada ya Ujerumani ambapo wanaungana na wenyeji Qatar.

,086,780

# JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 16/10/21 | 17:00 | Southampton vs Leeds | 2.40 | 3.52 | 2.82 |
| 02. 16/10/21 | 17:00 | Blackburn vs Coventry | 2.81 | 3.11 | 2.52 |
| 03. 16/10/21 | 17:00 | Millwall vs Luton Town | 2.30 | 3.20 | 3.06 |
| 04. 16/10/21 | 17:00 | Girona vs Huesca | 2.44 | 2.87 | 3.16 |
| 05. 16/10/21 | 19:15 | Las Palmas UD vs Tenerife | 2.51 | 2.95 | 2.95 |
| 06. 16/10/21 | 19:30 | Levante vs Getafe | 2.56 | 2.91 | 3.11 |
| 07. 16/10/21 | 21:30 | Malaga vs Zaragoza | 2.53 | 2.97 | 2.92 |
| 08. 17/10/21 | 13:30 | Cagliari vs Sampdoria | 2.72 | 3.37 | 2.56 |
| 09. 17/10/21 | 14:00 | Swansea vs Cardiff | 2.44 | 3.06 | 2.96 |
| 10. 17/10/21 | 16:00 | Everton vs West Ham | 2.38 | 3.42 | 2.92 |
| 11. 17/10/21 | 16:00 | Bordeaux vs Nantes | 2.78 | 3.13 | 2.59 |
| 12. 17/10/21 | 16:00 | Udinese vs Bologna | 2.36 | 3.35 | 3.00 |
| 13.17/10/21 | 17:00 | Leganes vs Valladolid | 2.46 | 2.97 | 3.02 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### ALHAMISI - 14 - OKTOBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1864 | Zenit II SP vs Krasava | 2.96 | 3.39 | 2.16 |
| 14:00 | 3383 | Zvezda ST Petersburg vs FC Kairat Moscow | 2.66 | 3.28 | 2.42 |
| 14:00 | 5312 | Kolomna vs FC Znamya Noginsk | 2.90 | 3.34 | 2.22 |
| 14:30 | 1198 | Beijing Guoan vs Sichuan Jiuniu | 1.37 | 4.64 | 6.58 |
| 14:30 | 1250 | Shanghai SIPG vs Xian Wolves | 1.06 | 9.67 | 19.34 |
| 14:30 | 2749 | Qingdao Huanghai vs Kunshan FC | 2.15 | 3.44 | 2.95 |
| 15:00 | 2321 | FC Fakel-M Voronezh vs Zenit Penza | 6.00 | 4.26 | 1.44 |
| 15:00 | 3809 | Baltika-Bfu Kaliningrad vs FC Tver | 5.63 | 4.17 | 1.48 |
| 15:00 | 4382 | Avangard Kursk vs Sokol Saratov | 6.97 | 4.46 | 1.38 |
| 15:00 | 5830 | Kvant Obninsk vs FC Saransk | 5.79 | 4.24 | 1.46 |
| 16:00 | 1215 | Tubas vs Markez Tulkarm | 2.42 | 3.25 | 2.67 |
| 16:00 | 2055 | Dynamo II vs Chertanovo Moscow | 1.28 | 5.21 | 8.10 |
| 16:00 | 2809 | Dinamo Briansk vs FC Salyut Belgorod | 1.86 | 3.64 | 3.54 |
| 16:00 | 4607 | Shabab AL Amari vs Markez Balata | 4.26 | 3.53 | 1.73 |
| 17:00 | 1453 | Queretaro U20 vs Tijuana U20 | 3.39 | 3.20 | 2.05 |
| 17:00 | 1466 | Lokomotiv II M vs Khimik Dzerzhinsk | 1.58 | 3.96 | 4.73 |
| 17:00 | 4156 | Peresvet Podolsk vs Strogino | 2.27 | 3.35 | 2.81 |
| 17:00 | 5132 | MS Kiryat Gat W vs Hapoel Nir Ramat Hasharon W | 1.14 | 7.16 | 12.58 |
| 17:00 | 5713 | FC Volna Nizhny Novgorod Oblast vs Shinnik Yaroslavl | 8.34 | 4.85 | 1.30 |
| 17:30 | 1679 | Arendal vs Rosenborg BK 2 | 1.06 | 9.75 | 19.50 |
| 17:30 | 4119 | Miercurea Ciuc vs FC Politehnica Iasi | 2.31 | 2.95 | 3.10 |
| 18:00 | 1346 | Metalac vs FK Zarkovo | 1.75 | 3.24 | 4.64 |
| 18:00 | 2215 | FC Murom Murom vs Yenisey 2 Krasnoyarsk | 2.19 | 3.34 | 2.95 |
| 18:00 | 4777 | Torpedo Vladimir vs FC Olymp-Dolgoprudny-2 | 3.77 | 3.43 | 1.86 |
| 18:30 | 3716 | TPS Turku vs EIF Ekenas | 1.30 | 5.02 | 7.73 |
| 19:00 | 3449 | Zalgiris vs Kedainiai Nevezis | 1.02 | 12.66 | 26.29 |
| 19:00 | 3502 | Ntnui vs Melhus | 2.36 | 3.77 | 2.46 |
| 19:00 | 5013 | Maardu Starbunker vs FC Elva | 1.16 | 7.50 | 12.83 |
| 19:30 | 1956 | Viking FK 2 vs Akra | 1.63 | 4.26 | 4.07 |
| 19:30 | 2124 | Linkopings W vs Vaxjo Dff W | 1.38 | 4.45 | 6.77 |
| 19:45 | 1159 | Bayern Munich W vs Kopparbergs Go W | 1.01 | 13.57 | 33.93 |
| 19:45 | 1961 | HB Koege W vs Barcelona W | 48.37 | 16.44 | 1.01 |
| 20:00 | 1323 | Hapoel Beer Sheva W vs AS Tel Aviv University W | 7.55 | 6.19 | 1.25 |
| 20:00 | 2065 | Jonkopings Sodra vs GIF Sundsvall | 2.58 | 3.33 | 2.68 |
| 20:00 | 3463 | Start 2 vs Express IL | 2.01 | 3.88 | 2.96 |
| 20:00 | 4688 | Vindbjart vs Donn | 1.28 | 5.80 | 7.16 |
| 20:00 | 5398 | FC Helsingor vs Esbjerg | 1.65 | 3.95 | 4.24 |
| 20:30 | 1206 | FC Hurth vs FC Pesch | 2.12 | 4.05 | 2.65 |
| 22:00 | 4673 | Lyon W vs SL Benfica W | 1.03 | 11.66 | 26.23 |
| 22:00 | 4960 | Arsenal W vs Hoffenheim W | 1.47 | 4.37 | 5.44 |
| 23:00 | 1653 | Bolivia vs Paraguay | 2.31 | 3.14 | 3.24 |

### IJUMAA - 15 - OKTOBA 2021

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 00:00 | 5650 | Colombia vs Ecuador | 1.68 | 3.66 | 5.21 |
| 01:00 | 3329 | Leones Negros Udg vs Club Celaya | 2.32 | 2.96 | 3.06 |
| 01:00 | 4350 | Sao Paulo vs Ceara CE | 1.72 | 3.34 | 4.65 |
| 01:00 | 4971 | Cuiaba MT vs Sport Recife | 2.05 | 2.91 | 3.78 |
| 02:30 | 2407 | Argentina vs Peru | 1.22 | 6.02 | 13.04 |
| 03:00 | 1656 | Chile vs Venezuela | 1.42 | 4.40 | 7.80 |
| 03:30 | 4005 | Brazil vs Uruguay | 1.52 | 4.00 | 6.60 |
| 04:00 | 1322 | Queretaro FC vs Club Tijuana | 2.30 | 3.15 | 3.10 |
| 05:00 | 1754 | Saprissa vs Guadelupe FC | 1.54 | 4.17 | 4.85 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.





# COURTOIS AISHUTUMU FIFA, UEFA

**LONDON,** England

GOLIKIPA wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Thibaut Courtois amelishutumu Shirikisho la Soka la Duniani (FIFA), na ile la Ulaya (UEFA), kwa kutojali tena wachezaji, baada ya kuongezeka kwa mashindano mengi na kuhoji umuhimu wa kutafuta mshindi wa tatu katika michuano ya Ligi ya Uefa.

Ubelgiji ilicheza na Italia katika kutafuta mshindi wa tatu kwenye michuano ya Ligi ya Mataifa ya Uefa, ambapo ilifungwa, kabla ya mchezo wa fainali ambao ulizikutanisha Ufaransa na Hispania. Na sasa Courtois ameishutumu FIFA na UEFA kwa kujali fedha pekee.

"Ni mchezo wa fedha tunapaswa tuwe wakweli kuhusu hili," alisema Courtois akiwaambia waandishi wa habari.

"Tumecheza huu mchezo ni kwa sababu ya UEFA, fedha ya ziada na mchezo wa ziada kwenye TV.

"Tutapata majeraha, hakuna anayejali wachezaji, baada ya msimu mrefu unatakiwa tena kucheza Ligi ya Uefa na utakuwa na wiki mbili za mapumziko hiyo haitoshi kwa wachezaji.

"Wanaweza kuchukizwa na Super League, lakini hawajali kuhusu wachezaji wanajali mifuko yao tu. Sisi siyo maroboti."




# Neymar akosolewa kutangaza kustaafu

**PARIS,** Ufaransa

KAULI ya Neymar kwamba, Kombe la Dunia 2022 linaweza kuwa ndiyo mwisho wake wa kuichezea Timu ya Taifa ya Brazil imekosolewa na nyota wa zamani wa Paris Saint-Germain, Jerome Rothem.

"Ujumbe wake wa hivi karibuni ni wa kutisha kwa PSG," alisema Rothen.

"Amekosa kujitolea kwenye klabu anafanya siyo sawa. Neymar ni mchezaji mzuri sana akiwa katika ubora wake, lakini tatizo ni kwamba anakosa ujasiri.

"Upendo alionao kwa Brazil ni dhahiri najua kwamba, anataka kushinda Kombe la Dunia.

"Nafasi yake ya mwisho itakuwa nchini Qatar mwaka ujao, lakini nadhani anapaswa kukabiliana na majukumu yake."

Neymar mwenye umri wa miaka 29 aliiambia DAZN, "Nadhani mwaka 2022 nchini Qatar itakuwa michuano yangu ya mwisho, kwa sababu sijui kama nitakuwa sawa kiakili na kimwili kukabiliana na soka tena.

# Michezo

Alhamisi Oktoba 14, 2021

Nipashe



Ronaldo afunguka ataka makubwa UKURASA 21



Mwakilishi wa Kampuni ya Star Times Tanzania, Juma Sharobaro (katikati), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni tano kwa nahodha wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), Amina Ally, kama zawadi baada ya timu hiyo kutwaa ubingwa wa mashindano ya Kombe la COSAFA 2021 yaliyofanyika nchini Afrika Kusini. **PICHA: BMT**

# SIMBA: TUTAIVAA JWANENG KIBABE

## Mipango na mikakati yakamilika lakini yaahidi...

**Na Saada Akida**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba wameendelea kujiimarisha kuelekea mchezo wao wa mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Jwaneng Galaxy ya Botswana kwa kufanya programu maalumu kwenye idara zake zote huku pia ikijiandaa na hali ya hewa ya baridi.

**Simba itashuka ugenini Botswana Jumapili kuwakabili Jwaneng Galaxy huku ikiwa na kumbukumbu za kutolewa kwenye hatua ya robo fainali ya michuano hiyo msimu uliopita.**

Kikosi hicho cha Simba kinatarajiwa kuondoka nchini kuelekea Botswana kesho tayari kwa mechi hiyo ya kwanza na baadaye kurejea jijini kwa ajili ya mchezo wa marudiano utakaochezwa Oktoba 24, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Kocha Msaidizi wa Simba, Thierry Hitimana, aliliambia gazeti hili kikosi chake kiko vizuri na wanashukuru kwa sasa hawana mchezaji hata mmoja ambaye ni majeruhi.

Hitimana alisema wakati wakiendelea kufanyia kazi mbinu za kiufundi uwanjani kwa kuzingatia ubora na madhaifu ya wapinzani wao, lakini wanajipanga kukabiliana na hali ya hewa watakayokutana nayo ugenini.

"Tumejiandaa vizuri kimbinu na kiufundi, pia tumeshajua tutaenda kucheza kwenye joto kali, tumeanza kulifanyia kazi hilo na kuzoea hali hiyo kabla ya kuondoka kuelekea Botswana," alisema kocha huyo.

Alisema wapinzani wao wana kikosi kizuri na kiuhalisia si timu ya kubeza na hali hiyo wanaendelea kujiimarisha ili kutowapa nafasi ya kutengeneza mashambulizi ambayo yataleta madhara.

"Katika hizi mechi ambazo tumecheza tumeona jinsi gani tulikuwa tukitengeneza nafasi na kushindwa kuzitumia, lakini mtu wa kutengeneza nafasi ya mwisho (namba 10,8) (awali alikuwa Clatous Chama aliyeuzwa), tayari yupo mtu ambaye amepewa jukumu hilo na kuna matarajio makubwa ya kufanya vizuri kwenye mchezo wetu huu," alisema Hitimana.

Wakati huo huo, Bodi ya Ligi (TPLB), imetangaza mchezo kati ya Simba dhidi ya Polisi Tanzania sasa utachezwa Oktoba 27, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini badala ya Oktoba 20, kama ilivyotangazwa hapo awali.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa TPLB, Almasi Kasongo, alisema jana bodi hiyo imefanya mabadiliko hayo kutokana na Simba kupata changamoto ya usafiri wa haraka wa kurejea nchini baada ya kumaliza mchezo wake wa kimataifa huko nchini Botswana.

Kasongo alisema Simba iliandika barua kuomba hivyo na wamekidhi kanuni mpya za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, hivyo mechi hiyo imesogezwa mbele.

"Bodi ya Ligi ni ya klabu. Ipo kwa kuzisaidia klabu, hasa inapokuja suala la mechi kama hizi za kimataifa. Na pia kanuni inaruhusu, hivyo bodi ikakubali ombi lao na utaona kuwa mechi imepangwa kuchezwa Oktoba 27, lengo ni kutoweka viporo kwenye ligi msimu huu, kwa hiyo itachezwa mapema," alisema Kasongo.

Aliongeza bodi imejipanga kuhakikisha msimu huu, timu zote zinacheza mechi sawa na kuondoa mrundikano wa viporo kama ilivyokuwa katika msimu uliopita.

## Samia: Twiga Stars mmetupa heshima

**Na Saada Akida**

WAKATI Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, akisema Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), zaidi ya Sh. milioni 50 zimepatikana kwa ajili ya kuipa zawadi timu hiyo iliyonyakua ubingwa wa mashindano ya COSAFA.

Rais Samia alisema amefurahi sana kuona Twiga Stars imeiwakilisha vyema Tanzania katika mashindano hayo na baada ya kurejea jijini Dar es Salaam, atakutana na nyota hao na kuwapa zawadi kwa sababu ya ushindi walioupata.

"Nawafuatilia, hongereni sana, nimemwagiza Katibu Mkuu ale nanyi leo, lakini nami nikija Dar nitawaita tuonane, hongereni sana na mmetuheshimisha Tanzania, hongereni na ninawatakia kila la kheri," alisema Rais Samia baada ya kupiga simu kwa Katibu wa Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo, Dk. Hassan Abbas wakati wa hafla ya kuwapongeza Twiga Stars iliyofanyika jijini juzi usiku.

Alisema kwa ushindi huo, wizara yame imeahidi kutoa kiasi cha Sh. milioni 20 huku akiongeza wamepokea mwaliko wa kwenda kutembelea mbuga ya Serengeti wakati wowote utakaofaa kwa ajili ya kuwapa mapumziko wachezaji.

Wengine walioahidi kutoa zawadi kwa Twiga Stars ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa EFM, Majizo ambaye atakabidhi Sh. milioni mbili, Wakala wa Serikali wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Sh. milioni tatu, Benki ya Biashara Tanzania (NBC), Sh. milioni 10, PSSF itatoa Sh. milioni mbili, Star Times (Sh. milioni tano) huku SBC wameahidi kutoa vinywaji wanavyozalisha.

Benki ya CRDB itatoa Sh. milioni 11, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Haki Miliki (COSOTA), kila mmoja Sh. milioni moja, Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe (Sh. milioni 1.1) na Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo Sh. milioni moja.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >